

**KUCHUNGUZA VIPENGELE VYA FANI KATIKA MASHAIRI YA
KISWAHILI: ULINGANISHI NA ULINGANUZI WA MASHAIRI YA
EUPHRASE KEZILAHABI NA HAJI GORA HAJI**

ABDOULHA MANSOUR ALI HASSAN

**TASNIFU YA KISWAHILI KWA MINAJILI YA KUTUNUKIWA SHAHADA
YA UZAMILI (MA. KISWAHILI) KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA
JAMII, YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2013

UTHIBITISHO

Aliyetia saina hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasinifu hii iitwayo:
Kuchunguza Vipengele vya fani katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganishi na ulinganuzi wa Mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji, na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digirii ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....
Sheikh, Professa, Dkt. T.S.Y.Sengo

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKIMILIKI

Haki ya kunakili tasunifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, Sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali ya kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama yote au sehemu ya Tasunifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Utafiti, Uchapishaji na Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

IKIRARI

Mimi **Abdolha Mansour Ali**, nathibitisha kuwa Tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digirii yoyote.

.....
Sheikh, Professa, Dkt. T.S.Y.Sengo

(Msimamizi)

.....
Tarehe

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa baba yangu **Mansour Ali** na marafiki zangu wote ambao kwa hakika wamejitoa kwa hali na mali katika kufanikisha malengo yangu ya kitaaluma ambayo yamenifikisha hatua hii ya kutunukiwa **Shahada ya Uzamili** katika Kiswahili.

SHUKURANI

Kwa hakika si kazi rahisi kuwataja na kuwashukuru kwa majina wote waliochangia kukamilika kwa utafiti huu. Hata hivyo, napenda kutumia fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wote ambao kwa njia moja ama nyingine wamewezesha kukamilika kwa utafiti huu. Wafuatao wanastahili shukurani za kipekee.

Kwanza, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, aliyenijaalia afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Sheikh, Professa, Dkt. T.S.Y.Sengo kwa msaada wake usio na kikomo uliowezesha kukamilika kwa utafiti huu. Kwa hakika alijitoa sana katika kuniiongoza, kunishauri, kunikosoa na kunielekeza katika hatua mbalimbali za utafiti wangu huu. Hivyo, ilinilazimu kutumia muda mwingi kutafakari na kufanyia kazi maelekezo yake yaliyosaidia kukamilika kwa utafiti huu. Nakushukuru sana Mzee Sengo na nakutakia kila la kheri katika maisha yako wewe binafsi pamoja na familia yako.

Tatu, natoa shukurani zangu za dhati kwa mfadhili wangu wa masomo ambaye ni Serikali ya Watu wa Libya kwa kujitoa, na kuniwezesha kwa kunilipia gharama za masomo yangu ya uzamivu na gharama za kujikimu katika kipindi chote cha masomo yangu.

IKISIRI

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu ambalo lilikuwa ni kuchunguza vipengele vya fani katika mashairi ya Kiswahili kwa kufanya ulinganishi na ulinganuzi wa mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji. Lengo hili limejumuishwa katika utafiti huu ili kuweza kuona kama kuna kufanana na kutofautiana kwa vipengele vya kifani katika mashairi ya kisasa na yale ya kimapokeo. Vilevile, tukaona ni busara japo kwa ufupi kueleza ama kudokeza dhamira mbalimbali zinazowasilishwa katika aina hizi mbili za ushairi yaani ushairi wa kisasa na ule wa Kimapokeo. Ili kufanikisha malengo ya utafiti huu tumekusanya data kwa kutumia mbinu za maktabani na kufanya uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa kuongozwa na mkabala wa kimaelezo kama inavyoonekana katika sura ya nne ya tasnifu hii. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, mashairi ya Euphrase Kezilahabi na yale ya Haji Gora Haji yanaonesha kutofautiana kwa vipengele vya kimuundo katika matumizi ya vina na mizani, kibwagizo, muundo wa tarbia katika beti za shairi zinatokeza sana katika ushairi wa Haji Gora Haji kuliko mashairi ya Euphrase Kezilahabi. Mashairi ya Euphrase Kezilahabi hayatumii kabisa vipengele hivi. Kwa upande wa kufanana kwao, tumeona kwamba, wote wawili wanatumia lugha ya mkato, taswira, wahasika pamoja na ucheshi. Vilevile, tumbaini kwamba Kezilahabi na Haji Gora Haji wanazungumza juu ya dhamira ambazo zinasawiri hali halisi ya maisha ya jamii ya Kitanzania na hata kwingineko duniani.

YALIYOMO

UTHIBITISHO.....	ii
HAKIMILIKI.....	iii
IKIRARI	iv
TABARUKU.....	v
SHUKURANI	vi
IKISIRI	vii
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 UTANGULIZI.....	1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti	1
1.2 Tatizo la Utafiti	4
1.3 Malengo ya Utafiti.....	5
1.3.1 Lengo Kuu.....	5
1.3.2 Madhumuni Mahususi.....	5
1.4 Maswali ya utafiti	6
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.6 Mipaka ya Utafiti.....	7
1.7 Vikwazo vya Utafiti.....	8
1.7.1 Utatuzi wa Vikwazo.....	8
1.8 Mpango wa Tasinifu	8
1.9 Hitimishi	9
SURA YA PILI.....	10
2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI.....	10

2.1 Utangulizi.....	10
2.2 Dhamira katika ushairi wa Kezilahabi	10
2.3 Mbinu za Kisanaa Katika Ushairi wa Kezilahabi	16
2.4 Ushairi wa Haji Gora Haji	21
2.5 Hitimishi.....	27
SURA YA TATU	28
3.0 NADHARIA ZA UTAFITI	28
3.1 Utangulizi.....	28
3.2 Nadharia ya Simiotiki	28
3.3 Nadharia ya Umaksi.....	30
3.4 Hitimishi.....	31
SURA YA NNE.....	32
4.0 MBINU ZA UTAFITI.....	32
4.1 Utangulizi.....	32
4.2 Utenzi wa Kazi za Kutafiti.....	32
4.3 Usanifu wa Utafiti	33
4.4 Populesheni na Sampuli ya Utafiti.....	33
4.4.1 Sampuli na Usampulishaji.....	34
4.4.2 Usampulishaji Nasibu Tabakishi.....	34
4.4.3 Sampuli Lengwa.....	35
4.4.4 Sampuli Nasibu Kutegemea Fursa	35
4.5 Vyanzo vya Data.....	35
4.5.1 Data za Msingi	36
4.5.2 Data za Upili	36

4.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data	36
4.7 Uchambuzi wa Data	37
4.8 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti	37
4.8.1 Usahihi wa Data	37
4.8.2 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti	38
4.8.3 Maadili ya Utafiti	38
4.9 Hitimishi	38
SURA YA TANO	40
5.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI	40
5.1 Utangulizi	40
5.2 Muundo Katika Ushairi	40
5.2.1 Vina na Mizani Katika Ushairi	43
5.2.2 Matumizi ya Kibwagizo	46
5.3 Mandhari Katika Ushairi	49
5.4 Matumizi ya Misimbo Katika Ushairi	53
5.5 Matumizi ya Mafumbo Katika Ushairi	57
5.6 Matumizi ya Lugha ya Taswira	59
5.7 Matumizi ya Wahusika Kifasihi Simulizi	61
5.8 Matumizi ya Ucheshi Katika Ushairi	64
5.9 Mwingiliano Matini	67
5.10 Udokezi Kuhusu Dhamira	68
5.11 Rushwa Katika Jamii	73
5.12 Hitimishi	75

SURA YA SITA.....	77
6.0 HITIMISHI, MUHTASARI WA MAPENDEKEZO	77
6.1 Utangulizi.....	77
6.2 Muhutajari	77
6.3 Hitimishi.....	79
6.4 Mapendekezo	80
MAREJELEO	81
VIAMBATISHI.....	85

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Ushairi wa Kiswahili ni sanaa kongwe inayopiga hatua ya maendeleo siku hata siku, kutokana na maendeleo ya mwanadamu katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Mabadiliko ama maendelo katika nyanja hizi yanaufanya ushairi wa Kiswahili nao kubadilika ili kuendana na mabadiliko haya na kuweza kuyasawiri kama inavyotakikana. Wamitila (2008) anaeleza kwamba, mabadiliko katika sayansi na teknolojia kwa mfano yameifanya fasihi ya Kiswahili (ushairi ukiwemo) kubadilika kimaumbo na kimaudhui. Kubadilika kimaumbo katika utafiti huu maana yake ni kubadilika katika vipengele vya fani ya ushairi. Fani ya ushairi iliyobadilika na tunayoiongelea hapa ni ile ya kutunga mashairi ambayo hayafuati urari wa vina na mizani kama afanyavyo Kezilahabi.

Wamitila (2008) anaeleza kwamba mabadiliko hayo ya kutunga mashairi ya kisasa ndiyo hasa yanaendana na maisha ya sasa ya jamii. Jamii ya sasa ni mchafu koge ambapo kila kitu kinafanywa kwa vurugu vurugu tu na hakuna utaratibu wowote. Anasema, kwa mfano; utaona katika jamii mtu mzima anambaka mtoto mdogo ambaye hajafikisha hata mwaka mmoja, rushwa na ufisadi unatendeka kwa kasi iliyokithiri wizi na ujambazi, uchawi pamoja na fitina kutaja mambo machache tu. Mambo yote haya yanahitaji aina ya fasihi ambayo itaweza kuyasawiri kama yalivyo na ama yanavyojitokeza. Aina hiyo ya fasihi si nyingine, bali ni ile isiyofuata kanuni zilizowekwa ama zilizokuwepo katika enzi za mababu zetu. Kwa mfano, hata

ukitazama aina ya muhiska aliyetumiwa na Shaaban Robert katika riwaya zake utaona kwamba, ni mhusika mkwezwa ambaye kumuona katika maisha ya siku hizi ni vigumu. Watunzi wa riwaya za siku hizi wameliona hilo na kwamba aina ya muhusika anayetumika katika kazi zao ni muhusika jumui (Mlacha na Madumulla, 1991).

Kama riwaya imekubali mabadiliko hayo ni kwa nini ushairi nao usikubali mabadiliko hayo? Bila shaka ni lazima kuyakubali mabadiliko hayo na kuyafanya sehemu ya fani yake kwa sasa. Kwa wanamapokeo ushairi hauwezi kubadilika na kuacha kanuni zake (Masamba, 2003). Ushairi unaweza kubadilika katika kueleza maudhui lakini si kanuni kwani kanuni pamoja na sheria ndivyo vitu vinavyolitambulisha jambo fulani na bila kuwapo kanuni hizo basi jambo hilo halitatambulika tena kwa sifa yake ya asili (Kandoro, 1978). Kwa maana hii, shairi ni lazima liendeleo kutungwa kwa kufuata urari wa vina na mizani ndivyo litakuwa shairi bora la Kiswahili, kwa sababu urari wa vina na mizani ndiyo uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili (Mayoka, 1984).

Mabadiliko yanayoelezwa katika upande wa maudhui ya ushairi wa Kiswahili ni yale yaliyoelezwa na Topan (1974) kwamba kwa sasa ushairi wa Kiswahili umekuwa ni sanaa pana inayohusisha si tu watu wa mwambao peke yao bali pia watu kutoka bara. Kama hivyo ndivyo, ni dhahiri kwamba, ushairi huo utakuwa si tu tena unaeleza masuala ya watu wa mwambao peke yao bali pia na yale ya wabara. Inasadikika kwamba, huko kale ushairi wa Kiswahili ulikuwa na dhima ya kuburudisha na kuwapamba watu mashuhuri katika jamii wakiwemo Wafalme na

Watemi katika jamii mbalimbali hasa ile ya Waswahili. Hata hivyo, kwa kipindi tulichonacho hivi sasa, kinaonesha kwamba, bado ushairi unatumika katika kuwasifu na kuwapamba watu mashuhuri katika jamii kwa kiasi fulani. Kwa upande mwingine, ushairi wa Kiswahili umekuwa ukitumiwa kama chombo cha kuwakosoa viongozi kutokana na matendo yao wanayoyafanya badala ya kuwasifu kwa maovu yao dhidi ya wananchi. Hili linaweza kupimwa kwa kutazama ushairi wa kimapokeo uliotungwa na wanamapokeo kwa vile akina Kandoro halafu unaulinganisha na ule wa Kezilahabi ama Mulokozi na Kahigi. Ni dhahiri utaiona tofauti katika maudhui na dhamira zinazoelezwa kupitia aina hizo mbili za utunzi wa mashairi.

Ingawa ushairi wa kisasa umekubalika na kuendelea kutumika katika tasnia mbalimbali ikiwemo ile ya taaluma, wanamapokeo walio wengi bado wanapinga kwamba, ushairi wa kisasa si ushairi wa Kiswahili. Saadan Kandoro kwa mfano: katika enzi hizo aliwahi kumueleza Mwalimu Nyerere, Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupiga marufuku utunzi wa mashairi aina ya kisasa (Mulokozi katika Mazungumzo, 2009).

Sengo (2012, katika mazungumzo) kwa upande wake haupingi ushairi wa kisasa kwa kuwapo kwake ila anasisitiza kwamba, asili ya ushairi wa Kiswahili ni lazima itambuliwe na iheshimiwe. Anaendelea kueleza kwamba, fasihi ina kwao na ushairi wa Kiswahili una kwao kama ilivyo ushairi wa kisasa nao una kwao. Hivyo, si sahihi kuchanganya mambo kwa kudai kwamba, ushairi wa Kiswahili ni ule wa mapokeo na kisasa pia. Kwa maelezo haya ni dhahiri kwamba, ushairi wa Kiswahili ni ule wa kimapokeo na ushairi wa Kisasa ni aina nyingine kabisa ya ushairi.

Gora katika mazungumzo yake na Said (2010) anaonekana kutokutambua kuwapo kwa ushairi wa Kiswahili wa kisasa na kudahili kwamba, kamwe hakuna aina kama hiyo ya ushairi wa Kiswahili. Kwa mujibu wa maelezo yake ni kwamba, aina hiyo ya utunzi inaonesha namna watunzi hao wasivyokuwa na ujuzi katika utunzi wa mashairi. Kwake yeye, shairi ni lazima liwe na urari wa vina na mizani ndiyo liitwe shairi na kama halina vitu hivyo basi si shairi bali ni kitu kingine kabisa.

Andanenga katika mahojiano yake na Chuwa (2011) anashangaa kuona aina ya ushairi wa kisasa imeanza kushika mizizi hata katika baadhi ya nyimbo za *bongo fleva*. Anashangaa pia kuona kuwa, hata vyombo vya habari vimeshamiri katika kupiga nyimbo hizo. Kwa hali hii Andanenga anadai kwamba, ushairi wa Kiswahili upo hatarini kupotea. Kwa mtazamo na msimamo wake ushairi pekee ni ule wa kimapokeo na ushairi wa kisasa hauwezi kuwa ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo, kutokana na maelezo hayo kuhusu ushairi wa kisasa na ule wa kimapokeo kuwa bado yana ukinzani. Tumeona kwamba, kutokana na ukinzani huo wa kimaendeleo, ipo haja ya kufanya utafiti wa kina kwa kulinganisha na kulinganua viengele mbalimbali vya kishairi baina ya aina hizo mbili za ushairi. Tunafanya hivi kwa kumchanganua mmoja wa washairi wanaopinga kuwapo kwa mashairi ya kisasa kuwa ni sehemu ya ushairi wa Kiswahili. Mshairi huyu si mwingine bali ni Haji Gora Haji. Katika utafiti wetu, tunaulinganisha na kuulinganua ushairi wake wa ule wa Euphrase Kezilahabi- muasisi wa ushairi wa kisasa.

1.2 Tatizo la Utafiti

Haji Gora Haji katika mazungumzo yake na Said (2010) anadai kwamba hakuna kitu kinachoitwa ushairi wa kisasa katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili. Anaendelea

kueleza kwamba, yeyote anayetunga aina hiyo ya ushairi si mbobezi katika fani ya ushairi wa Kiswahili na anapaswa kukaa darasani ili afundishwe kuhusu fani hiyo na afunzike. Kauli hizi za Gora Haji Gora zimetusukuma kufanya utafiti linganishi baina ya ushairi wake (wa Kimapokeo) na ule wa Euphrase Kezilahabi (wa Kisasa) ili kubaini kilichopo kwenye ushairi wake tofauti na kile kilichopo katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kukubali au kukanusha kwamba, hakuna kitu kinachoitwa ushairi wa kisasa. Vilevile, tumeamua kufanya utafiti huu ili kubainisha bayana tofauti na ufanano wa ushairi wa Kiswahili wa kimapokeo na ule wa kisasa kuwa, nyakati zote kumekuwapo na malumbano pamoja na madai kwamba, aina hii si ushairi na hii ndiyo ushairi, bila ya kuwapo na maelezo ya kina yanayotafautisha aina hizo za ushairi. Kwa kufanya hivi tunaweza kuziba pengo hili pana la kiutafiti.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu moja na malengo mahususi matatu. Malengo hayo ni kama yanavyoainishwa hapa chini.

1.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kulinganisha na kulinganua ushairi wa kisasa na wa kimapokeo wa Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji mutawalia.

1.3.2 Madhumuni Mahususi

- (a) Kueleza kutofautiana kwa vipengele vya fani katika ushairi wa Haji Gora Haji na ule wa Euphrase Kezilahabi.

- (b) Kuainisha kufanana kwa vipengele vya fani baina ya ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji.
- (c) Kudokeza dhamira zinazojitokea katika mashairi ya Kezilahabi na yale ya Haji Gora Haji.

1.4 Maswali ya utafiti

- (a) Ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji unatofautiana katika vipengele gani vya kifani?
- (b) Kuna ufanano gani katika vipengele vya kifani baina ya ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji?
- (c) Ni dhamira zipi zinazochomoza katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa una umuhimu katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:

Utafiti na kujisomea: Utafiti huu utakuwa na umuhimu wa kutumika kama rejeleo muhimu katika tafiti za baadaye kuhusiana na ushairi wa kimapokeo na ule wa kisasa. Vile vile, utafiti huu utatumika kama kitabu ama rejeleo kwa wanafunzi wa ngazi za shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu katika taaluma za fasihi ya Kiswahili.

Kiutamaduni: Utafiti huu utaonesha masuala ya kiutamaduni katika jamii za mwambao na jamii za bara kupitia diwani za *Kimbunga*, *Karibu Ndani* na *Dhifa*.

Kwa kuzibainisha tamaduni hizo itakuwa rahisi kwa msomaji na mtafiti ama mhakiki yoyote yule kuzielewa kwa undani pale anapotaka kutumia tamaduni hizo katika maandishi yake.

Kihistoria: Utafiti huu utakuwa sehemu mojawapo ya muendelezo wa maendeleo ya historia ya Kiswahili tangu kupatikana kwa uhuru mpaka kufikia leo. Baada ya kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika, historia ya ushairi wa Kiswahili ilianza na mgogoro wa ushairi wa Kiswahili na sasa tunaandika kuhusu mambo yatokanayo na mgogoro huo.

Kinadharia: Utafiti huu ni muhimu katika kuimarisha nadharia ya ushairi na kimapokeo na ile ya ushairi wa kisasa. Nadharia hizi zitaimarika kutokana na utafiti huu kuyaeleza masuala ya muhimu yanayoshadadiwa na kila nadharia kati ya hizo mbili za ushairi wa Kiswahili.

Katika ngazi ya elimu ya sekondari utafiti huu utakuwa na umuhimu kwa watunga sera na mitaala ya elimu kwamba, wanapotunga mitaala hiyo kuhusu fasihi ya Kiswahili kwa ujumla na ushairi mahususi wazingatie mambo gani yanayopaswa kuingizwa katika mitaala hiyo. Baadhi ya mambo hayo watayatoa katika tasnifu hii.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unashughulikia masuala ya kifani kwa undani na udokezi kidogo wa dhamira katika mashairi ya Euphrase Kezilahabi na yale ya Haji Gora Haji. Masuala haya yatalinganishwa na kulinganuliwa ili kukamilisha malengo ya utafiti wetu. Katika utafiti huu hatutachunguza masuala yasiyo ya kifasihi kuhusu maisha binafsi

ya watunzi hawa wawili ingawa kwa kiasi kidogo yanaweza kuhusishwa hapa na pale ili kutumiza malengo ya utafiti.

1.7 Vikwazo vya Utafiti

Kikwazo kikubwa katika utafiti huu kilikuwa ni lugha hasa lugha ya kishairi. Mtafiti ni mzaliwa wa Libya na lugha mama yake ni Kiarabu na Kiswahili ni lugha yake ya pili. Kwa hali hii ilimpa taabu kupata maana za mashairi mbalimbali kutokana na ukweli kwamba, lugha ya mashairi kuwa ni ya mafumbo, taswira na ishara isiyoeleweka kwake (mtafiti) kwa urahisi.

1.7.1 Utatuzi wa Vikwazo

Msimamizi wa utafiti huu alimpatia mtafiti msaidizi ambaye ni mtaalamu wa Kiswahili wa ngazi ya shahada ya kwanza ambaye ndiye aliyemsaidia mtafiti kudadavua matumizi ya ishara, picha, taswira na mafumbo katika mashairi ya washairi teule. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliweza kukusanya data zilizosaidia kujibu maswali ya utafiti wake.

1.8 Mpango wa Tasinifu

Tasinifu hii ina jumla ya sura sita. Sura ya kwanza ni ile ambayo inaeleza masuala mbalimbali yanayohusiana na utangulizi wa utafiti ikiwemo usuli na tatizo la utafiti. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi kuhusiana na mada ya utafiti. Katika sura hii tumepitia kazi tangulizi mbalimbali kuhusu ushairi wa Euphrase Kezilahabi na kisha, Haji Gora Haji. Sura ya tatu inahusu nadharia za utafiti huku sura ya nne ikieleza juu ya mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data. Sura ya tano inahusu

uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Sura ya sita inaeleza kuhusu muhutasari, hitimishi na mapendekezo.

1.9 Hitimishi

Sura hii imetoa utangulizi kuhusu utafiti huu ambapo lengo kuu la kufanyika kwa utafiti huu limebainishwa. Sambamba na lengo kuu pia yamebainishwa madhumuni mahususi ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti. Mambo haya yote yameonesha ulazima wa kufanyika kwa utafiti huu. Vilevile, katika sura hii tumeeleza kuhusu umuhimu wa utafiti, mipaka, vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Huu ni utafiti linganishi ambao unalinganisha ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Gora Haji Gora. Vipengele vinavyo linganishwa ni vile vya fani kwa kiasi kikubwa na maudhui kwa kudokezwa tu. Katika sura hii tunafanya mapitio ya kazi tangulizi ili kuona watafiti wa mwanzo wanazungumza nini kuhusiana na mashairi ya Euphrase Kezilahabi nay ale ya Haji Gora Haji. Ili kuifanya sura hii kuwa toshelevu tumepitia kazi tangulizi kwa kila mshairi halafu ndio tukatoa hitimishi. Hata hivyo, tunakiri kwamba kazi za Euphrase Kezilahabi zimeandikiwa kwa kiasi kikubwa ikilignanishwa na zile za Haji Gora Haji. Hii inatokana na ukweli kwamba, Euphrase Kezilahabi alileta mapinduzi katika fasihi ya Kiswhaili ushairi ukiwepo, hivyo kuwafanya wanafasihi walio wengi kumakinikia zaidi kazi zake ili kuyachunguza mabadiliko/mapinduzi aliyoyaleta. Ukweli huu unatufanya tuanze kutazama kazi tangulizi katika ushairi wa Kezilahabi.

2.2 Dhamira katika ushairi wa Kezilahabi

Senkoro (2010) katika mihadhara ya Umahiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama anavyonukuliwa na Omary (2011) anaeleza kwamba, Euphrase Kezilahabi hakuleta mabadiliko katika muundo wa ushairi peke yake bali katika dhamira pia. Wakati ushairi wa kimapokeo uliandika mashairi yenye kurejelea katika kuadili na kuadibu kama dhamira zao kuu. Euphrase Kezilahabi ameandika juu ya kukosoa mifumo mbalimbali ya kisiasa, uongozi na uchumi nchini kama sehemu ya kuonesha namna kizazi kipya kisivyoridhika na maamuzi mengi yatolewayo ama yafanywayo na

viongozi wa umma. Asemapo/awasiilishapo dhamira hizo kwa jamii iliyokusudiwa Euphrase Kezilahabi hutumia lugha ya kawaida kabisa lakini yenye kuhitajia uzingativu wa hali ya juu ili kuweza kuelewa na kudadavua maana zinazopatikana kupitia lugha hiyo.

Uelewa wa Senkoro kuhusu ushairi wa Euphrase Kezilahabi unaungwa mkono na Mulokozi (1975) pale anapoeleza kwamba, usomapo ushairi wa Euphrase Kezilahabi unaweza kudhani kwamba, unasoma lugha ya kawaida itumiwayo na wanajamii katika maisha yao ya kila siku. Kwa mfano katika shairi la *Mke wa Waziri* (uk. 13) Kazilahabi, anasema:

*Sikiliza Monika,
Sisi tumezoea vituko vya wakubwa,
Huyo mumeo anatoka kijiji jirani
Tulimuona akilambwa na mbwa
Alipomaliza kujisaidia
Na alikimbia siku ya tohara
Sasa naye avuta kidevu shingo upande
Kama beberu tayari kupigana
Wewe Monika
Twende ufukweni kuogelea
Tuone hiyo cheni ya dhahabu*

Ubeti huu wa shairi unaeleza dhamira kama vile uongozi mbaya na utabaka katika jamii. Ukigeukia lugha iliyotumiwa unaona kwamba ni lugha ya kawaida mno ambayo inahitaji msomaji kufikiri zaidi ili aweze kupata dhamari tulizozieleza hapo awali. Uandishiwa aina hii wa Kezilahabi umetuvutia kufanya utafiti linganishi ili kuona yeye anafananaje ama kutofautianaje na Haji Gora Haji.

Msokile (1992) anaeleza kwamba, Euphrase Kezilahabi ameandika juu ya dhamira mbalimbali na kubwa zaidi ikiwa ni ujenzi wa jamii mpya. Anaendelea kueleza

kwamba, maelezo yaliyo mengi katika diwani ya *Karibu Ndani* (1988) yanaonesha kukosoa maamuzi ya kuanzisha Azimio la Arusha, kwamba halikuleta tija na faida yoyote kwa mwananchi wa kawaida, zaidi ya kuongeza umasikini. Ananukuu shairi la *matumaini* (uk.07) kuwa:

*Akiyumbayumba
Na sarawili zee mawinguni
Kama mlevi mwenye mguu mmoja
Nilimuona
Akitoka magharibi kwenda mashariki
Kisha akaanguka baharini kwa kishindo.*

Uelewa wa Msokile (1992) ni muafaka katika kuwezesha utafiti huu kufanikiwa kwa sababu unaonesha kwamba, Kezilahabi ni mtu wa kukata taama na kutokana na hilo anatoa mahitimishi ambayo si sahihi. Kwa mfano, si kweli kwamba, Azimio la Arusha halikuleta maendeleo yoyote kwa wananchi wa Tanzania. Azimio la Arusha lilisaidia kutoa fursa kwa wananchi kupata elimu, huduma za afya, maji na makazi bila kuchangia gharama zake, huku serikali ikilipia gharama hizo kwa asilimia mia moja. Hali hii ilipasaidia wananchi masikini kupata huduma zote muhimu bila taabu wala shida na hivyo kuondoa utabaka mkubwa wa matajiri na masikini ulioanza kuonekana baada tu ya kupatikana kwa uhuru.

Hivyo basi, kutoa maelezo kwamba Azimio la Arusha halikuwa na faida yoyote kwa wananchi si kweli ingawa tunakubaliana kwamba, Azimio la Arusha lilikabiliwa na vikwazo pamoja na hima mbalimbali. Utafiti huu umefanywa ili kuonesha namna Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji walivyoyaeleza mambo haya kama yanavyotokeza katika sura ya nne ya tasinifu hii.

Nao Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba, Euphrase Kezilahabi anaeleza dhamira ambazo zinaiakisi jamii ya Watanzania wa wakati huu. Anaendelea kueleza kwamba ushairi wa Euphrase Kezilahabi hauzingatii matumizi ya vina wala mizani lakini unaeleza juu ya matatizo yatokanayo na utandawazi na kuifanya jamii ya Watanzania kuendelea kuwa masikinini. Wanaendelea kueleza kwamba, ukisoma ushairi wake utaiona dhahiri hasira aliyonayo dhidi ya wakoloni/wageni pamoja na viongozi ambao ndiyo hutoa fursa hizo za uwekezaji kwa wageni hao ambao huwekeza katika mashamba/ardhi madini, hoteli, utalii na katika sekta nyinginezo. Faida kubwa itokanayo na uwekezaji huu huchukuliwa na wawekezaji huku wananchi wakiachiwa umasikini usio kifani.

Uelewa huu wa Njogu na Chimerah (1999) unaungwa mkono na Wamitila (2008) pale anaposema kwamba, ushairi wa Euphrase Kezilahabi haujakosewa kupewa jina la ushairi wa kisasa kwa sababu unaeleza juu ya matatizo yanayoikabili jamii kwa sasa. Mawazo haya yanaenda mbali na kuonesha kwamba, matatizo kama vile rushwa, ufisadi, umasikini, migomo ya wafanyakazi na matatizo yao yanaelezwa katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi. Uelewa huu umesaidia kukamilisha utatifi wetu baada ya kuuchukua na kuutumia katika kulinganisha na kulinganua na ushairi wa Haji Gora Haji ili kuona mfanano na tofauti zinazojitokeza kuhusiana na dhamira hizi.

Frolova (2003) anaandika makala yake yenye mada isemayo “Euphrase Kezilahabi Muhiishaji wa Ushairi wa Kiswahili,” (Euphrase Kezilahabi the Renewal of Kiswahili Poetry). Katika makala hii pamoja na mambo mengine anaandika kwamba, Euphrase Kezilahabi katika *Karibu Ndani* (1988) anaandika kuhusu

dhamira zinazoeleza masuala ya mtu binafsi na si dhamira za kisiasa kama alivyofanya katika *Kichomi* (1974). Mawazo haya yalipingwa vikali na Omary (2011) alipoonesha kwamba, hakuna shaka kuwa Euphrase Kezilahabi ni muhishaji wa ushairi wa Kiswahili lakini si kweli kwamba hazungumzii masuala ya kisiasa katika *Karibu Ndani* (1988) bali anazungumzia masuala ya kisiasa tena kwa kiwango cha hali ya juu kabisa. Katika kujibu hoja hii Omary (2011) alitumia baadhi ya mashairi yaliyoelezwa na Frolova (2003) kwamba hayazungumzii masuala ya kisiasa na kuonesha namna mashairi hayohayo yanavyoisawiri dhamira hiyo. Sababu kubwa aliyoigundua Omary (2011) ya kumfanya Frolova kutoa hitimishi alilolitoa ni kwamba, hakuongozwa na nadharia yoyote ile ya uhakiki wa kifasihi katika uandishi wa makala yake hiyo. Kwa upande wake Omary (2011) alitumia nadharia ya Simiotiki ambayo ilifanikisha kuonesha kwamba Kezilahabi anazungumzia masuala ya kisiasa katika ushairi wake.

Kwa upande wa pili tunamuona Frolova (2003) alikuwa sahihi kutoa hitimishi alilolitoa kwa sababu hii ni kazi ya fasihi ambayo daima haina jibu ama mtazamo mmoja. Mulokozi (1996) anasema kwamba, kazi bora ya fasihi ni ile ambayo haina jibu moja. Kila msomaji wa kazi hiyo anapoisoma hupata maana yake tofauti na ile aliyoipata mwenzake. Anaendelea kueleza kwamba, mtunzi anaweza kutunga akiwa na maana fulani kichwani mwake lakini wasomaji wake wakaibua maana mbalimbali nyingi zaidi kuliko alivyodhani yeye. Kwa mtazamo huu, ni dhahiri kwamba Frolova (2003) ana haki ya kueleza hivyo alivyoeleza. Hata hivyo, haikuwa haki yake kufunga milango kwa kutoa kauli kwamba masuala ya kisiasa hayajitokezi katika ushairi huo uliopo katika *Karibu Ndani* (1988).

Hoja nyingine ya Frolova (2003) iliyosaidia kutoa mwelekeo wa utafiti huu ni ile inayodai kwamba, Euphrase Kezilahabi anaonesha kurudisha imani kwamba maendeleo yatapatikana nchini kupitia diwani yake ya *Karibu Ndani* (1988) kinyume na aliyoonesha kukata tamaa katika diwani yake ya mwanzo itwayo *Kichomi* (1974). Mawazo haya tumeyachukua na kuyatumia katika utafiti wetu ingawa tunapinga kwamba si kweli kuwa Kezilahabi alionesha kukataa taama ya kupatikana maendeleo kwa taifa katika diwani ya *Kichomi* (1974). Yapo mashairi katika diwani hiyo ambayo Euphrase Kezilahabi anaelezea matumaini yake juu ya upatikanaji wa maendeleo nchini.

Hata hivyo, tumeuchukua uelewa huu na kuutumia katika kulinganisha na kulinganua ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji katika kipengele hiki cha kukata ama kutokata tama juu ya upatikanaji wa maendeleo kwa taifa. Omary (2011) aliofanya utafiti juu ya siasa katika ushairi wa Kezilahabi. Katika utafiti wake huo, anaonesha kwamba, Kezilahabi anaeleza dhamira za kisiasa zihusianazo na makundi mawili. Kundi la Kwanza ni siasa za Ujamaa na Kujitegemea zinazotokeza kwa kiasi kikubwa katika *Karibu Ndani* (1988). Kundi la pili ni siasa za Kiliberali zinazojitokeza katika diwani ya *Dhifa* (2008).

Katika dhamira zinazohusiana na Ujamaa na Kujitegemea dhamira kuu ni ujenzi wa jamii mpya. Katika siasa za Kiliberali dhamira kuu ni masuala ya kidemokrasia na uhuru wa mwanadamu kutoa maoni yake na kushirikishwa katika maamuzi. Mawazo haya ya Omary (2011) ni muafaka katika kusukuma mbele utafiti wetu tumeyachukua na kuyatumia katika kuainisha dhamira zinazohusiana na masuala ya

siasa za Ujamaa na zile za Kiliberali na kisha tukazitofautisha na kuzilinganisha na zile za Haji Gora Haji.

Katika watafiti wote tuliowapitia hapo juu tumebaini kwamba hakuna hata mmoja aliyeleza kwamba Euphrase Kezilahabi amezungumzia dhamira gani nyingine tofauti na masuala ya kisiasa; Utafiti huu umefanywa ili kuona kama Euphrase Kezilahabi anazungumza aina nyingine ya dhamira tofauti na masuala ya kisiasa na kisha kuzifananisha na kuzitofautisha dhamira hizo na zile za Haji Gora Haji. Baada ya maelezo/mapito ya kazi tangulizi kuhusiana na dhamira katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi sasa tutazame kazi tangulizi zinazoeleza juu ya matumizi ya mbinu za kisanaa katika ushairi wa Kezilahabi.

2.3 Mbinu za Kisanaa Katika Ushairi wa Kezilahabi

Mbinu za kisanaa ni ufundi anaoutumia mwandishi katika kuijenga kazi yake iweze kuwasilisha dhamira kwa jamii iliyokusudiwa huku ikitoa hamu kwa wasomaji ama jamii hiyo kuisoma kazi hiyo tena na tena. Euphrase Kezilahabi tofauti na washairi wa kimapokeo aliibua mtindo wake wa kutunga mashairi yasiyofuata urari wa vina na mizani. Tapon (1974) anaandika kwamba, Euphrase Kezilahabi ni miongoni mwa wanataaluma mashuhuri wanaostahili kupongezwa kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuuletea ushairi wa Kiswahili mtindo mpya. Topan (1974: ix) anaeleza hivi:

Kezilahabi anaufuata mtindo mpya wa kunadika, mashairi ya kifasihi. na hii ndio njia ya kwanza ya kukuza fasishi ya Kiswahili kwa kuuletea mtindo mpya wa kutunga mashairi.

Mawazo haya tunayakubali na kwamba yanasaidia kutoa njia ya kufanikisha utafiti wetu. Kwanza yanaeleza juu ya mtindo mpya ambao utafiti huu umeutumia katika

kuulinganisha na kuutofautisha na ule wa Haji Gora Haji. Pili umetusaidia kufahamu kwamba, Kezilahabi amechangia katika kukuza ushairi wa Kiswahili. Hoja hii ya pili ilituvutia sana na kisha kutuwezesha kutambua kwamba, inafaa kutumika katika kulinganisha na kulinganua ushairi wa Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji ili kuona kama kisemwacho na Topan (1974) kinajitokeza katika ushairi wa Haji Gora Haji.

Tunasema hivi kwa kuwa, mahali pengine ambapo Topan (1974: xi) anasema:

Ulikuwa wakati hapo zamani ambapo mshairi wa Kiswahili alikuwa mwenyeji wa mwambao na visiwani tu. Hivyo mashairi ya siku hizo yaliandikwa, kufuatana na mila, desturi na sheria za kipwani. Mawazo yaliyomo humo pia yalihusu maisha na utamaduni wa kimwambao.

Tunakubaliana na mawazo ya Topan (1974) kwamba ushairi wa Kiswahili umepiga hatua mbele zaidi katika mawanda juu ya yale unaoyaeleza ikilinganishwa na kipindi cha nyuma kabla ya ujio wa watu wa bara kati uandishi wa mashairi hayo. Miongoni mwa hao waandishi wa bara ni Euphrase Kezilahabi. Hata hivyo, mawazo ya Topan (1974) hapo juu yanaonekana kujikanganya kwa msingi kwamba; kama ushairi wa Kiswahili ulieleze masuala ya mila, desturi na sheria za kipwani si ndio kazi ya ushairi ya kuusawiri utamaduni wa jamii yake. Kuja kwa watunzi wa ushairi wa bara na kuanza kutunga mashairi yanayochanganywa ubara na upwani bado yataendelea kuitwa mashairi ya Kiswahili au ni mashairi mseto. Hali hii ilitutia hamasa ya kufanya utafiti huu ili kuona namna ushairi unaoandikwa na Mswahili Haji Gora Haji unavyofanana ama kutofautiana na ule wa Mbara Euphrase Kezilahabi katika kueleza mambo ya mila, desturi na sheria za jamii za Kiswahili.

Naye Mayoka (1984) katika katibu chake kiitwacho *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka* anadai kwamba, Euphrase Kezilahabi hawezi kuwekwa katika kundi la

waandishi wa ushairi wa Kiswahili kwa sababu anachoandika si ushairi. Anaenelea kuandika kwamba, utanzu wa ushairi una miiko na kanuni zake na moja ya kanuni hizo ni lazima shairi liwe na urari wa vina na mizani. Anachoandika Euphrase Kezilahabi kinakosa sifa hii ambayo kwa mujibu wa Mayoka- vina na mizani ni uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Tukiyatazama mawazo haya tunaona kwamba yanapingana na yale yaliyotolewa na Topan (1974) kwa kuwa yale ya Topan yana ukubali ushairi wa Euphrase Kezilahabi kuwa ni ushairi wa Kiswahili na haya ya Mayoka (1984) yanaupinga ushairi huo.

Mayoka kama anavyofahamika yeye ni mfuasi mkuu wa mashairi ya kimapokeo, ambapo Haji Gora Haji naye anaangukia katika kundi hilo ingawa yeye (Haji Gora Haji) hatajwi sana katika mgogoro wa ushairi wa Kiswahili. Kwa hiyo ni sawa na kusema kwamba, Haji Gora Haji anaandika ushairi unaofuata urari wa vina na mizani. Kwa ujumla maelezo haya yametoa kichocheo cha kuwezesha utafiti huu kukamilika kwa misingi kwamba, unadokeza mambo ambayo ndio tuliyoyatumia katika kutofautisha na kufananisha ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji. Sura ya nne imeonesha ni namna gani mashairi ya washairi hawa yanavyotofautiana katika matumizi ya vina na mizani.

Mulokozi na Kahigi (1979) ni wafuasi wa mashairi huru yasiyofuata urari wa vina na mizani. Katika maelezo yao, wanasema kwamba ni kweli kuwa Euphrase Kezilahabi hatungi mashairi yake kwa kufuata urari wa vina na mizani lakini usomapo mashairi yake utaona anatumia midundo ama ridhimu ambayo hutoa msisitizo kwa msomaji juu ya dhamira ama wazo ambalo msanii anataka hadhira ilipate. Chuwa (2011)

anayaunga mkono maelezo haya pale anapotumia nadharia ya elimu mitindo na kufanikiwa kuonesha kwamba, Euphrase Kezilahabi ni gwiji katika matumizi ya ridhimu katika ushairi wake. Kwa mantiki hiyo anaongeza kwamba, kila sauti katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi inamchango mkubwa katika kulielewa shairi hilo.

Vilevile, anaendelea kueleza kwamba, ili kuweza kuelewa vizuri ushairi wa Kezilahabi ni lazima msomaji ama mhakiki awe na ujuzi wa nadharia za uhakiki wa kifasihi ambao utamsaidia kuzielewa sauti/ridhimu zinazojitokeza katika ushairi husika na kisha kuzitolea maana. Ufahamu huu tumeuchukua na kuutumia katika kulinganisha ushairi wa Haji Gora Haji na ule wa Euphrase Kezilahabi kwa minajili ya kuonesha athari ya vina, mizani na ridhimu katika kuibua maudhui katika mashairi yao.

Wamitila (2008) anaeleza kwamba, si jambo la kawaida kukutana na matumizi ya wahusika katika ushairi wa mashairi mafupi mafupi kama yale watungayo Haji Gora Haji na Euphrase Kezilahabi. Wahusika hujitokeza katika tendi na tenzi ambazo ni aina ya mashairi yaelezayo mambo kwa urefu. Hata hivyo, anasema kwamba Kezilahabi anatumia wahusika katika mashairi yake na aina ya wahusika anaowatumia kwa wingi ni wale na kifasihi simulizi. Wahusika hao ni wadudu, wanyama madubwana, mazimwi, mashetani na binadamu kwa uchache. Anaendelea kueleza kwamba matumizi ya wahusika hawa huenda sambamba na kupewa sifa na uwezo wa kutenda kama binadamu na hivyo kusaidia kuibua dhamira mbalimbali. Maelezo haya ya Wamitila (2008) yametupatia uelewa zaidi ambao hasa umetuweza kupata mambo ya kulinganisha na kutofautisha baina ya ushairi wa Haji Gora Haji

na ule wa Kezilahabi. Dhana ya wahusika imewasilishwa katika sura ya nne kama inavyojitokeza katika kazi za washairi hawa wawili tuliowashughulikia.

Naye Senkoro (2006) anaeleza kwamba, ushairi wa Euphrase Kezilahabi una matumizi makubwa ya mbinu za kifasihi simulizi, jambo ambalo linaufanya kuwa na sura ya Kiafrika zaidi kuliko ile ya Kimagharibi kama ilivyo katika baadhi ya kazi za fasihi. Anaendelea kuongeza kwamba, wapo waandishi wengine ambao wameandika kazi za riwaya na tamthilia, zilizo pewa jina la fasihi za majaribio. Lakini, Senkoro anasema, Euphrase Kezilahabi ameandika na ushairi pia kwa kutumia mbinu za kifasihi simulizi kama vile ucheshi, matumizi ya picha, ishara, taswira taharuki na marudiorudio na kadhalika. Kwa kufanya hivi Senkoro (2006) ametudokezea vipengele vya kisanaa ambavyo vinajitokeza katika ushairi wa Kezilahabi nasi, bila ajizi tumevitumia vipengele hivi katika utafiti wetu. Tumeonesha namna vipengele hivi vinavyotumiwa kwa kufanana ama kutofautiana baina ya Haji Gora Haji na Euphrase Kezilahabi. Tofauti na makala ya Senkoro (2006) ambayo haikuwa na lengo la kueleza juu ya vipengele hivyo kwa kina utafiti wetu umezama na kumakinikia vipengele hivyo kwa udhati wake. Tumefanya hivi kwa sababu hili lilikiwa ndiyo lengo kuu la utafiti wetu.

Omary (2011) amefanya utafiti juu ya siasa katika ushairi wa Kezilahabi pamoja na vitu vingine alitaja kwa ufupi kuhusu mbinu za kisanaa zilizotumiwa na Kezilahabi katika kuibua masuala hayo ya kisiasa. Mbinu alizozitaja ni pamoja na ucheshi, wahusika, usimulizi na matumizi ya lugha ya ishara, taswira na picha. Ingawa hakueleza kwa undani kuhusiana na vipengele hivi kwa kuwa halikuwa lengo lake

kuu la utafiti wake, ametusaidia kufahamu baadhi ya mbinu anazoitumia Euphrase Kezilahabi katika kuibua dhamira na maudhui katika ushairi wake. Tumevichukua vipengele hivi/mbinu hizi za kisanaa na kuzitumia katika utafiti wetu kwa minajili ya kulinganisha na kulinganua ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji.

Mapitio haya ya kazi tangulizi kuhusu ushairi wa Euphrase Kezilahabi yanaonesha kwamba, Euphrase Kezilahabi ni mtunzi wa mashairi ya kisasa yasiyofuata urari wa vina na mizani lakini ushairi huo umewavutia wataalamu wengi wa fasihi ambao baadhi yao wamempa jina la “Mhuishaji wa ushairi wa Kiswahili (Frolova, 2003). Pamoja na yote haya kuelezwa, hakuna utafiti uliofanyika kumtofautisha na kumfananisha Kezilahabi na mshairi yoyote wa kimapokeo katika utunzi wake wa mashairi. Utafiti huu umefanyika kwa ajili ya kulinganisha na kutofautisha mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji katika utunzi wao wa mashairi. Yafuatayo ni mapitio ya kazi tangulizi kuhusu Ushairi wa Haji Gora Haji.

2.4 Ushairi wa Haji Gora Haji

Ushairi wa Haji Gora Haji si maarufu sana katika tahakiki na tafiti katika ngazi ya Chuo Kikuu. Hii ni kwa sababu, yeye hakuwepo katika masuala ya mgogoro wa ushairi wa Kiswahili wa miaka ya 1970 ikilinganishwa na akina Jumanne Mayoka, Saadan Kandoro, Sudi Andanenga na Mathias Mnyampala kuwataja wachache. Vilevile, kazi zake za ushairi kama vile *Kimbunga* ni ya hivi karibuni tu ambapo mwaka 1994 ndipo alipotoa chapa ya kwanza. Ingawa yeye hakuwepo katika kundi la wanamapokea wakati wa mgogoro lakini naye anaandika mashairi yenye kufuata,

urari wa vina na mizani na kamwe hautambui ushairi wa kisasa kama sehemu ya ushairi wa Kiswahili. Kutokana na ukweli huu kuhusu ushairi wa Haji Gora Haji haina maana kwamba ushairi wake hauna umashuhuri katika ngazi nyingine za elimu nchini Tanzania.

Nyangine na Masebo (2002) wanasema kwamba, mshairi Haji Gora Haji ni mshairi wa kimapokeo aliyetunga kitabu cha *Kimbunga* (1994) ambacho kinatumika katika elimu ya sekondari katika masomo ya uhakiki wa kifasihi nchini Tanzania. Wanaendelea kueleza kwamba, usomapo mashairi yake utakutana na matumizi ya mizani na vina ambavyo vinaonekana katika beti zote za shairi. Kwa mfano, matumizi ya vina na mizani yanaonekana katika shairi la *Kimbunga* (1994:01) pale anaposema:

*Kimbunga mji wa Siyu, kilichawahi kufikaSi kwa yule wala huyu,
ilikuwa patashika kimeing'owa mibuyu, mizazi kunusurika nyoyo
zilifadhaika.*

Tunapolitazama shairi hili tunona matumizi ya vina kati “yu” na vina mwisho “ka” vikitumiwa katika ubeti huu. Shairi lote la “Kimbunga” limeandikwa kwa kutumia kina mwisho “ka” huku vina kati vikibadilika kutoka ubeti mmoja na mwingine. Mfano huu unatufanya tukubaline na maelezo ya Nyangwine na Masebo (2002) kwamba, ushairi wa Haji Gora Haji umeandikwa kwa kuzingatia urari wa vina na mizani. Mawazo haya tumeyachukua na kuyatumia katika kutofautisha na kuufananisha ushairi huu na ule wa Kezilahabi kama ilivyowasislishwa katika sura ya nne ya tasnifu hii. Sengo (1994) anaeleza kwamba Haji Gora Haji ni mtaalamu katika matumizi ya lugha ya mafumbo ambayo ndiyo muafaka katika utunzi wa mashairi. Anasema:

Kimbunga, katika lugha ya kawaida, ni neno linaloashiria dhana ya tufani kali liwezalo kuvunja nyumba, kuezua vipaa na kusababisha maafa ya namna kwa namna. Katika tungo hizi za Bwana Haji Gora Haji kimbunga ni fumbo badala ya kuathiri kila kitu kutokana na nguvu zake, chenyewe huathiri baadhi tu ya vitu na vingine hunusurika. Mbuyu unapongolewa na mnazi kunusurika; majabali yanapobirukizwahirukizwa, meli zikadidimia na ngarawa kuokoka; mangorofa yakarushwa angani na vibanda vikalimika; ni wazi kwamba si kimbunga cha kawaida ingawa tunajua na tunakiri kuwa fimbo ya mnyonge ni Mwenyezi Mungu mwenyewe.

Maelezo haya ya Sengo yanaonesha kwamba, shairi la *Kimbunga* limedhamiriwa kutoa fumbo kali kuhusiana na suala la kuleta mapinduzi na mabadiliko katika jamii hasa pale wananchi wa kawaida wanapoamua kuliondoa tabaka tawala madarakani. Vile vile, fumbo hili limetumika kurejelea masuala kama vile uongozi mbaya na utabaka uliopo katika jamii. Maelezo ya Sengo hayakuwa marefu sana kwa kuwa haikuwa sehemu ya malengo yake kueleza kwa kina kuhusu matumizi ya lugha katika ushairi wa Haji Gora Haji. Utafiti wetu umefanywa kwa undani zaidi katika kuchunguza kufanana na kutofautiana baina ya mashairi ya Kezilahabi na Haji Gora Haji kwa namna iliyosaidia kujibu maswali ya utafiti huu.

Sengo (1994) anaendelea kueleza kwamba, Haji Gora Haji ni mtu muhimu sana katika kukuza na kukiendeleza Kiswahili. Katika kufanya hivyo, Haji Gora Haji anaeleza umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika maendeleo ya jamii na pia anaeleza kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili. Sengo (1994) anasema:

Kiswahili ni shairi liitwalo “Kiswahili” ambalo kituo chake ni lugha ya Kiswahili, wenyewe ni wa mwambao. Ama Bwana Haji Gora Haji angekuwako katika malumbano yetu ya kitaaluma ambamo Bwana T.S.Y. Sengo (1988) alizingirwa na kuzongwa, huenda walumbi wake akina Madumulla, Kihore, Senkoro na wengine wangesisimka namna tofauti kidogo.

Kwa hili, tunaungana mkono na Sengo (1994) kwamba Haji Gora Haji anania kuu ambayo ni njema katika kukikuzi na kukieneza Kiswahili. Tumeyachukua mawazo haya na kuyalinganisha na yale ya Kezilahabi kuhusiana na kuikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Ni dhahiri kwamba Kiswahili kinaasili yake ambayo ni mwambao wa pwani ya Afriaka Mashariki na kwamba kwa sasa kina watumiaji wengi kutoka katika makabila mbalimbali nchini Tanzania jambo linaloonesha kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, kuwapo na watumiaji wa lugha ya Kiswahili kutoka makabila mbalimbali si sababu ya kueleza kwamba, watu hao (makabila mbalimbali) nao ni Waswahili. Ni Waswahili wa kuzungumza lakini si Waswahili kwa utamaduni wake (Sengo, 1994). Mawazo haya tumeyafanyia kazi katika sura ya nne ya tasnifu yetu.

Sengo (1994: viii) anaeleza kwamba Haji Gora Haji ameandika mashairi mazuri ya kuwataka viongozi kuwa waadilifu katika kuwatumikia wananchi na kamwe wasiwaibie wananchi rasilimali zao kupitia rushwa na ufiadi. Anaeleza kuwa:

Chaka ni fumbo la tahakiki dhihi ya tabia mbaya. Yumkini ni tabia hasi za uongozi au za maisha kwa jumla. Mtunzi anaonya kuwa hilo tegemeo lao hao waovu limeshatambulikana. Bora waovu wayaache hayo kwani kiumbe mwando hayati, majuto huya kinyume”

Katika ubeti huu Sengo (1994) anaonesha kwamba, wananchi wameshawashitukia viongozi wala rushwa na wanawataka kuacha tabia hiyo mara moja kwa kuwa inarudisha nyuma maendeleo ya taifa na kuongeza umasikini kwa wananchi. Ingawa Sengo (1994) hakwenda mbali zaidi katika kuichambua dhamira hii kwa undani, ametupatia mwelekeo katika uchambuzi wetu. Tumeyachukua mawazo haya na kuyafanyia kazi iliyowezesha kukamilika kwa utafiti huu.

Njogu na Chimerah (1999) katika kitabu chao cha ufundishaji wa fasihi nadharia na mbinu wameitaja tu diwani ya *Kimbunga* (1994) pale walipokuwa wameleza masuala ya utunzi wa mashairi kwa kuzingatia urai wa vina na mizani. Kutokana na kudokeza kwao huku juu ya diwani hii, wamesaidia katika kukazia uelewa wetu kwamba Haji Gora Haji ni mtunzi wa mashairi ya kimapokeo. Kwa ufahamu huu tumeyachukua mawazo haya na kuyatumia katika kulignanisha na kulinganua mashairi ya Haji Gora haji na Euphrase Kezilahabi katika utunzi wao wa mashairi.

Selemani na Mtimbo (2004) walifanya uchambuzi kuhusu dhamira zinazojitokeza katika diwani mbali mbali za ushairi mojawapo ikiwa ni diwani ya *Kimbunga* (1994). Katika uchambuzi wao wanaeleza kwamba, dhamira ya malezi, wosia na maongozi mema vinajitokeza kwa kiasi kikubwa katika mashairi ya Haji Gora Haji. Wanaendelea kusema kwamba, usomapo mashairi haya utabaini kwamba, mengi ya mashairi hayo yanazungumzia umuhimu wa kuwa na malezi mema kwa jamii kuanzia kwa watoto, vijana, wazee viongozi, wasio viongozi na kadhalika. Hoja hii tunaiunga mkono kwa kuwa ni suala lisilopingika kwamba, washairi wengi wa kimapokeo waliandika mengi ya mashairi yao kwa kuzingatia dhamira hii adhimu. Hata hivyo, wahakiki hawa hawakwenda mbali zaidi katika kuchambua dhamira hizo kwa undani badala yake wameeleza kwa kugusiagusia tu. Utafiti huu umelitazama jambo hili kwa undani kwa kulinganisha na kulinganua mashairi ya Haji Gora Haji na Euphrase Kezilahabi ili kuona kwamba, ni kwa kiwango gani aina hizi mbili za ushairi zinalitazama suala la malezi, wasia na maongozi mema.

Said (2010) katika mazungumzo yake na bwana Haji Gora Haji waliyoyafanya katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili anaeleza kwamba, mshairi huyu anakataa

katakata kwamba hakuna kitu kinachoitwa ushairi wa kisasa na kwamba ushairi ni ule unaofuata urari wa vina na mizani. Anasema kwamba yeye (Haji Gora Haji) hajawahi kusikia kwamba kuna kitu kinaitwa jahazi la zamani na jahazi la kisasa; meli ya zamani na meli ya kisasa; kanga ya zamani na kanga ya kisasa, iwaje hali hiyo itokee katika ushairi. Anaendelea kueleza kwamba, wanaotunga mashairi na kuyaita ya kisasa ni wale ambao hawawezi kutunga mashairi kwa kuzingatia kanunia zake kama zilivyoainishwa na Abeid (1954).

Mawazo haya yatolewayo na Said (2010) yametoa mchango muhimu kaika kuharakisha utafiti wetu kukamilika. Mawazo haya yametufanya tuchunguze kwa kina ushairi wa Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji ili tuone ni kwa vipi hasa unatofautiana mpaka Haji Gora Haji auone ushairi wa kisasa uandikwao na Euphrase Kezilahabi siyo ushairi.

Juma (2012) alifanya utafiti kuhusiana na ufundishaji wa ushairi wa Kiswahili katika shule za sekondari. Katika utafiti wake huo amebaini kwamba miongoni mwa vitabu vya ushairi vinavyotumika katika kufundishia ushairi katika shule za sekondari ni *Kimbunga* (1998). Anaeleza kwamba wanafunzi aliofanya nao usaili walimueleza kwamba diwani hii inaeleweka vizuri kwao kwa sababu walipata fursa ya kukutana na mtunzi wake bwana Haji Gora Haji ambaye aliwapatia ufafanuzi wa baadhi ya mashairi yake na hivyo kupata uelewa zaidi. Suala hili nalo tunakubaliana nalo kwamba pale mtunzi wa kazi ya fasihi anapotunga kazi yake huwa na maana fulani ambayo anataka hadhira yake ilipate. Hivyo basi, inapotokea fursa ya yeye mwenyewe kuielezea diwani hiyo basi inakuwa ni rahisi kwa hadhira kuielewa kazi hiyo kwa uharaka na wepesi zaidi.

Hata hivyo, tunaongeza kwamba wasomaji au wasikilizaji wa kazi ya fasihi nao wanayo nafasi yao katika kuibua dhamira mbalimbali kutokana na kazi ya fasihi iliyowasilishwa kwao. Kwa maana hiyo nasi pia kama wahakiki tumeweza kuibua maana mbalimbali kutoka katika mashairi ya Euphrase Kezilahabi na yale ya Haji Gora Haji kwa minajili ya kuweza kulignanisha na kulinganua utunzi wa mashairi yao. Mwandishi Eliott aliwahi kueleza kwamba kazi bora ya fasihi ni ile ambayo inaweza kuzalishwa maana nyingi na wasomaji wake ingawa mtunzi wa kazi hiyo alikuwa na maana yake alipoandika kazi hiyo ya fasihi.

2.5 Hitimishi

Sura hii imepitia kazi tangulizi kuhusiana na mada ya utafiti. Kazi hizi tangulizi zimewekwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni mapitio ya kazi tangulizi katika ushairi wa Euphrase Kezilahabi na kundi la pili ni lile la ushairi wa Haji Gora Haji. Sura hii imebaini kwamba, watafiti tangulizi hawa wametumia muda wao mwingi katika kueleza masuala ya kifani na maudhui yanayojitokeza katika kazi za wasanii hawa wawili bila kufanya uchunguzi wa kina katika kazi zao na badala yake wanagusagusa tu. Vile vile, hakuna hata mtafiti mmoja aliyethubutu kufanya ulinganishi baina ya ushairi wa Haji Gora Haji na ule wa Euphrase Kezilahabi. Utafiti huu umefanywa kwa undani zaidi katika kulinganisha na kulinganua ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji jambo lililosaidia kujaza pengo la kiutafiti liliyoachwa na watafiti watangulizi.

SURA YA TATU

3.0 NADHARIA ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inapitia nadharia kadhaa ambazo kwanzo zimetumika katika uchambuzi wa ushairi wa Euphrase Kezilahabi na ule wa Haji Gora Haji. Ni vema ikaeleweka wazi kwamba, utafiti wowote ule wa kifasihi ni lazima uongozwe na nadharia muafaka ili uweze kutoa majibu yanayokidhi malengo ya utafiti kama yalivyoorodheshwa na mtafiti. Nadharia ndiyo itoayo mwelekeo wa utafiti; mbinu, upitiaji wa kazi tangulizi na uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti wote hufanywa kwa kuongozwa na nadharia zilizoteuliwa na mtafiti. Kwa msingi huu utafiti huu umeongozwa na nadharia za Simiotiki na Umarx. Maelezo ya kina kwa kila nadharia yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo.

3.2 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuzihakiki kazi za kifasihi ambao unaangaza ishara za kifasihi katika kazi hizo. Nadharia hii kwa ujumla inajishughulisha na ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi (Wamitila, 2002:132).

Ishara zinazojitokeza katika kazi za fasihi huundwa na utunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Wamitila (2002) anaeleza kwamba, binadamu ni mtengenezaji na mnyambulishaji wa ishara mbalimbali zitumikazo katika kazi za fasihi. Wasomaji na watazamaji wa kazi za

fasihi hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya ishara hizo. Mawazo haya yanakamilishwa na yale ya Chandler (1992) aliposema kuwa, tunafikiri kwa kutumia alama. Alama hizo zinakuwa katika mfumo wa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, matendo na mtenda au yambwa. Anaendelea kueleza kwamba kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakipa fasiri kama kirejeele, yaani kinasimama kwa niaba ya kitu kingine badala ya chenyewe.

Wamitila (2002) anaendelea kueleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja (a signifier), yaani umbo ambalo alama inachukua na kirejeele (a signified), yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo. Kutokana na maelezo haya tunapata uelewa kuwa, kuna kitaja, na kirejeele ambapo mahusiano ya viwili hivyo ni ya kubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii husika. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kirejeele, lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na huelewana miongoni mwao. Bathes (1994) akaja na aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa Kimatukio, Kihemenitiki, Kiseme, Kiishara na Kirejelezi.

Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji kama ilivyo kwa baadhi ya washari wengine wanatunga mashairi yao kwa kutumia lugha ya picha, ishara, mafumbo, sitiari, na taswira kali haswa. Nadharia ya Simiotiki imetoa mwongozo muafaka katika kuzichambua aina zote hizo za matumizi ya lugha na kisha kuwezesha kufanikisha madhumuni ya utafiti huu. Nadharia nyingine ni ile ya Umaksi, nayo inaelezwa kama ifuatavyo.

3.3 Nadharia ya Umaksi

Msingi mkubwa wa nadharia hii unatokana na mawazo ya Karl Marx na Fredrich Engels. Karl Marx (1818-1883) anahusisha U-Maksi na Nyanja kama vile uchumi, historia ya jamii na mapinduzi (Wamitila, 2002:182). Kimsingi, mawazo ya Marx yanalenga kuwataka wanafasihi kuzitazama hali za jamii zao zilivyo na kuzitafutia ufumbuzi kwa maana ya kuzibadilisha kuliko kuzitafsiri tu.

Mawazo ya Karlmarx kuhusu historia na miundo ya kijamii yana nafasi kubwa katika nadharia hii. Umaksi ni falsafa ya Kiyakinifu hasa kwa kuwa pana msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali za kiyakinifu za maisha kama mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu. Umaksi hautegemezi mfumo wake wa kifalsafa kwenye dhana dhahania kama urembo, ukweli au ndoto bali anayetegemea kwenye uhalisi unaonekana (Wamitila, 2002:182). Mawazo haya yametusaikia kusukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, mashairi ya washairi teule huihakiki jamii katika uhalisia na udhahania. Mfumo wa maisha tulio nao leo ni ule ulioongeza tofauti kati ya walionacho na wasio nacho (utabaka) na kusababisha kuwapo kwa mgogoro wa kitabaka katika jamii za Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Wamitila (2002:183) anaeleza kwamba:

Wahakiki wa Ki-Marx wanaamini kuwa daima historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi – jamii. Itakumbukwa kuwa Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka ... Kitu cha msingi katika maisha ya binadamu ni kula na kunywa, kupata malazi na mavazi na mambo mengine.

Mambo haya ndiyo humfanya binadamu kupambana ili aweze kuyapata na kisha aweze kuishi maisha mazuri. Wakoloni kwa hakika hawakutoa fursa kwa wananchi

kuwa na maisha mazuri kwa kuwa daima waliwatumikisha kwa kazi nyingi malipo kidogo. Hali hii iliwafanya wananchi kufanya kila linalowezekana ili waipate haki yao ya uhuru na kisha kupanga mipango yao ya maendeleo itakayowaletea maendeleo. Usomapo ushairi wa Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji utabaini kwamba, uwanaharakati wa kitabaka ndio unaotawala sana katika mashairi hayo. Hivyo basi nadharia ya Umaksi imeongoza vema uchambuzi na uhakiki wa mashairi ya wateule hawa kama inavyoonekana katika sura ya tano ya tasinifu hii.

3.4 Hitimishi

Sura hii imewasilisha nadharia tatu ambazo zimeongoza utafiti huu. Nadharia hizo ni simiotiki na Umaksi. Kila nadharia imetoa mchango maridhawa katika kuhakiki mashairi ya washairi teule. Nadharia ya Simiotiki imesaidia katika kuainisha picha, ishara, taswira na ishara mbalimbali katika mashairi hayo. Nadharia ya Umaksi imesaidia katika kubainisha matabaka, unyonyaji, rushwa na ufisadi katika mashairi ya wawili hao.

SURA YA NNE

4.0 MBINU ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii ndiyo ambayo inawasilisha mbinu zilizotumika katika kukamilisha utafiti huu. Kothari (1992) anaeleza kwamba, utafiti wa kitaaluma ni wajibu ufanywe kwa kuzingatia mbinu, njia na taratibu zote za utafiti ili uweze kupata matokeo yasiyo na shaka kulingana na kile kilichokusudiwa kutafitiwa. Kwa kuwa utafiti wetu ni wa kitaaluma tumelazimika kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba, tunatumia mbinu sahihi za kuongoza utafiti huu. Mbinu hizo ni kama zinavyowasilishwa katika sura hii hapa chini.

4.2 Utenzi wa Kazi za Kutafiti

Utafiti huu unahusu fasihi kipengele cha ushairi na kwamba huu ni utafiti wa maktabani. Kwa kuwa ni utafiti wa maktabani tumelazimika kuteua kazi za washairi wawili ambao ni Haji Gora Haji na Euphrase Kezilahabi na kuzifanyia uhakiki na uchunguzi ili kujibu maswali ya utafiti huu. Kazi za washairi hawa zimeteuliwa kwa sababu zinatoka katika aina tofauti za ushairi; moja inatoka katika kambi ya wanausasa na nyingine inatoka kambi ya wanamapokeo. Kwa kuteua kazi hizi mbili zinazotoka katika makundi haya mawili tumeweza kukamilisha malengo ya utafiti wetu. Sababu nyingine iliyotufanya tuteue kazi hizi ni kutokana na kauli ya Haji Gora haji aliyoitoea katika mazungumzo yake na Said (2010) kuwa yeye hatambui kitu kinachoitwa ushairi wa kisasa. Kauli hii ilitusukuma katika kufanya utafiti wa aina hii. Kazi zilizoteuliwa ni *Kimbunga* (1994) iliyotungwa na Haji Gora Haji na *Karibu Ndani* (1988) pamoja na *Dhifa* (2008) zilizotungwa na Euphrase Kezilahabi.

4.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni ramani ama mchoro unaoonesha namna utafiti utakavyofanyika tangu katika kukusanya data mpaka kuwasilisha. Kuchambua na kujadili data za utafiti (Kothari, 2008). Utafiti huu umeteua mbinu ya uchunguzi kifani kwa kuteua kazi za washairi wawili. Kazi zilizoteuliwa ni *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008) zilizotungwa na Euphrase Kezilahabi na *Kimbunga* (1994) iliyotungwa na Haji Gora Haji. Euphrase Kezilahabi ni mtunzi mwenye diwani tatu mpaka sasa nasi tumepoendelea kuchagua diwani hizo mbili ambazo zinakaribiana kiwakati na ile moja tu ya *Kimbunga* aliyonayo/iliyo chapishwa ya Haji Gora Haji mpaka kufika sasa.

Babbie (1999) anaeleza kwamba, uchunguzi kifani ni aina ya usanifu ambayo inampa mtafiti muda na kutosha kulitafiti jambo moja kwa undani zaidi na kisha kuweza kulitolea mahitimisho stahiki. Mbinu hii pia inamsaidia mtafiti kutopoteza muda mrefu kwa kushughulikia kazi nyingi kwa wakati mmoja na badala yake anamakinikia kazi chache alizoteua (Furlong, na wenzake, 2000). Kutoka na umuhimu huu ndio maana tukaamua kuiteua mbinu hii ya usanifu na kuitumia katika utafiti wetu.

4.4 Populesheni na Sampuli ya Utafiti

Populesheni ni neno linalotumika kurejelea idadi ya watu, vitu ama jambo ambalo mtafiti anataka kulitafiti ili kutimiza malengo ya utafiti wake (Babbie, 1999). Kwa maana hiyo basi, populesheni ya utafiti huu ni vitabu vitatu vya ushairi viwili vikiwa ni vya ushairi wa kisasa na kimoja ni cha mashairi ya kimapokea pamoja na mashairi yake yote yaliyomo ndani ya vitabu hivyo. Mtafiti ameamua kuteua diwani hizi tatu

kwa sababu ndizo hasa zilizoweza kujibu maswali ya utafiti huu na kuweza kutimiza malengo yake.

4.4.1 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli inafasiriwa kama kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kutoka katika idadi kubwa ya wanajamii ama vitu vyovyote vile ambavyo mtafiti anataka kuvitafiti (Keys, na Wenzake, 1989). Ili kuwezesha uteuzi wa kundi hilo dogo kutoka katika kundi kubwa kufanikiwa zipo mbinu za aina mbali za kufanya usampulishaji. Kumbasi usampulishaji ndiyo kitendo chenyewe cha kufanya uteuzi wa sampuli ya utafiti husika (Newman, 2006). Usampulishaji katika utafiti huu umefanywa kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni usampulishaji nasibu tabakishi na usampulishaji nasibu kutegemea fursa.

4.4.2 Usampulishaji Nasibu Tabakishi

Usampulishaji Nasibu ni aina ya usampulishaji ambayo watafitiwa wote wana fursa sawa ya kuteuliwa kushiriki/kuhusishwa katika utafiti husika. Usampulishaji nasibu tabakishi ni usampulishaji unaofanywa baada ya kuwa panga watafitiwa ama vitafitiwa katika makundi ama madaraja mbalimbali na kisha watafitiwa ama vitafitiwa hivyo vina kuwa na nafasi sawa katika kuteuliwa. Yaani baada ya kutenga makundi ama madaraja hayo ndipo watafitiwa ama vitafitiwa huteuliwa kinasibu. Hii ndiyo maana ya usampulishaji nasibu tabakishi. Aina hii ya usampulishaji imetumika katika kufanya uteuzi wa diwani mbili za Euphrase Kezilahabi. Tulizipanga diwani zake tatu alizotunga kwa kuanza na ile ya mwanzo na kufuatiwa na za baada yake. Diwani hizo zilipangwa hivi:

1. *Kichomi* (1974)

2. *Karibu Ndani* (1988)
3. *Dhifa* (2008)

Baada ya kuzipanga namna hii ndipo tukabaini kwamba diwani namba 2 na 3 hapo juu zinakaribiana kwa karibu na diwani ya *Kimbunga* (1994) katika kipindi cha kutungwa kwake. Kwa hivyo tukaona kwamba hata dhamira za diwani hizo hazitatofautiana kwa kiasi kikubwa ingawa haziwezi kuwa sawasawa kwa kila hali na jinsi.

4.4.3 Sampuli Lengwa

Hii ni aina ya sampuli ambayo mtafiti anateua watafitiwa ama vitafitiwa akiwa amejiridhisha kwamba watafitiwa hao watampatia data itakayoweza kutimiza malengo ya utafiti wake (Yin, 1994). Aina hii ya usampulishaji imetumika katika kuiteua diwani ya *Kimbunga* (1994) ya Haji Gora Haji ambapo tulijiridhirisha kwamba itatusaidia kupata data za utafiti wetu na ndivyo ilivyokuwa.

4.4.4 Sampuli Nasibu Kutegemea Fursa

Sampuli nasibu kutegemea fursa ni aina ya sampuli ambayo inatoa fursa sawa kwa watafitiwa wote kujumuishwa katika utafiti pasina kuwapo upendeleo wa aina yoyote ile (Kothari, 2008). Aina hii ya usampulishaji imetumika katika uteuzi wa mashairi, beti za mashairi ama mishororo ya ushairi ambayo kila mtafiti alipokutana na kimoja kati ya hivyo ambacho kinahusiana na utafiti huu alikinukuu katika daftari la kukusanyia data tayari kwa uchambuzi.

4.5 Vyanzo vya Data

Utafiti huu umekusanya data za msingi na za upili ambazo ndizo zilihita jika ili kuweza kukamilisha malengo ya utafiti huu. Data hizi zilikusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali kama inavyoelezwa hapa chini.

4.5.1 Data za Msingi

Data za msingi hukusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yoyote yule kwa minajili kama ya utafiti huo unaofanyika hivi sasa (Kothari, 2008). Katika utafiti huu data za msingi zimekusanywa kutoka katika diwani mbili za Kezilahabi na diwani moja ya Haji Gora Haji. Data hizi zimekamilishwa na data za upili zilizokusanywa katika vyanzo kadhaa kama inavyoelezwa hapa chini.

4.5.2 Data za Upili

Hizi huitwa data fuatizi ama za ziada ambazo hutumiwa kujazilizia data za msingi ili kuweza kujibu maswali ya utafiti husika. Data hizi hukusanywa katika vyanzo kama vile vitabu, makala, tasnifu, majarida, wavuti, tovuti, mazungumzo, barua na kadhalika. Katika utafiti wetu tumesoma kazi mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti na kuweza kupata data za upili zilizozisaidia data za msingi katika kujibu maswali ya utafiti wetu.

4.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Baada ya kuwa tumekwisha ainisha vyanzo mbalimbali vya data hatua iliyofuata ni kukusanya data za utafiti. Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya kusoma kwa makini kazi zilizoteuliwa na kila tulipokutana na shairi ama beti au mshororo unaohusiana na kile tunachokitafiti basi tulikidondoa katika shajara/daftari letu maalumu na kisha kutumia katika uchambuzi wa data. Kothari (2008; Robson, 2007) anaiita mbinu hii kuwa ni ya uchambuzi wa kimaudhui. Kwa kuwa utafiti huu ni linganishi ilibidi tuandae madaftari mawili ambapo moja lilitumika kukanya data

kutoka katika mashairi ya Haji Gora Haji na daftari la pili lilitumika kukusanyia data zilizotoka katika mashairi ya Euphrase Kezilahabi.

4.7 Uchambuzi wa Data

Ili kufanikisha malengo ya utafiti wetu tumelazimika kufanya uchambuzi wa data tulizokusanya. Kothari (2008) anaeleza kwamba uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika kukamilisha malengo ya utafiti husika. Ni katika hatua hii ndipo utafiti hukamilika na kuonekana kuwa umeweza kufanikisha lile lililodhamiriwa na mtafiti.

Utafiti huu umetumia mbinu ya uchambuzi wa data wa kinaelezo kama ilivyoainishwa na Creswell na Wenzake (2006). Mkabaka huu unamtaka mtafiti kutoa maelezo kwa kila data yake kwa namna ambayo inajibu maswali ya utafiti wake. Kwa mfano katika utafiti huu uchambuzi wa data umefanywa kama ifuatavyo: Kwanza, tulianza kwa kuteua vichwa ama mada ambazo tutazitumia katika kulinganisha na kulinganua ushairi wa Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji. Baada ya hapo tulidondoa beti ama mshororo ambao unahusiana na mada tuliyoiteua na kuanza kufanya uchambuzi wetu. Uchambuzi huo ulifanywa kwa kutoa maelezo kwa kila dondoo kwa namna iliyowezesha kujibu maswali ya utafiti wetu.

4.8 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti

4.8.1 Usahihi wa Data

Usahihi wa data za utafiti huu unatokana na mbinu iliyotumika katika ukusanyaji wa data kutumiwa kama inavyopasa kutumiwa (Cohen, na wenzake, 2000; Furlong, na

wenzake, 2000). Mtafiti na msaidizi wake walitumia muda wa kutosha kusoma mashairi yaliyohusiana na mada ya utafiti kwa kurudia shairi moja zaidi ya mara tano. Kwa kufanya hivyo tuliweza kupata data zilizosaidia kujibu maswali ya utafiti huu kwa usahihi. Vile vile, mtafiti alikaa na msimamizi wake hatua kwa hatua ili kuona kama kuna mahali data zinaonekana kuwa si sahihi na kisha kuzirekebisha mpaka kufikia hatua inayoonekana hivi sasa.

4.8.2 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti

John (2004) wanaeleza kwamba, kuaminika kwa data za utafiti yaani matokeo ya utafiti kunatokana na uwezo na mbinu za utafiti kutoa majibu ama matokeo yale yale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile. Katika utafiti huu iwapo utarudiwa kwa kutumia mbinu zile zile ni dhahiri kwamba utatoa majibu yale yale. Hata hivyo tunakiri kwamba, hii ni kazi ya kifasihi ambayo inaweza kuchunguzwa na kutolewa maana na majibu tofauti tofauti kulingana na nia ya mtafiti. Hata hivyo kama mtafiti atatumia mbinu na nadharia zile zile basi nidhahiri kwamba matokeo hayatatofautiana kwa kiasi kikubwa.

4.8.3 Maadili ya Utafiti

Utafiti wowote ule wa kitaaluma ni sharti uzingatie maadali ya utafiti ili kutoa matokeo sahihi. Katika utafiti huu tumezingatia maadili ya utafiti ikiwa ni pamoja na kuomba na kupatiwa kibali cha kufanya utafiti huu katika ngazi stahiki.

4.9 Hitimishi

Katika sura hii tumeelza mbinu za utafiti pamoja na taratibu nyingine zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data. Taratibu hizi zimetusaidia kuufanya utafiti

huu kwa uharaka na umakini zaidi kwa sababu kila jambo lilielezwa bayana kwamba litafanyikaje na kwa utaratibu gani. Miongoni mwa taratibu hizo za utafiti zinatokeza katika sura hii ni pamoja na uteuzi wa kazi za utafiti, usanifu wa utafiti, populesheni na sampuli ya utafiti na vyanzo vya data za utafiti. Taratibu nyingine ni zile zinazohusu ukusanyaji na uchambuzi wa data, kuaminika, usahihi na maadili ya utafiti. Vipengele hivi kwa pamoja vimewezesha utafiti wetu kuonekana ulivyo hivi sasa.

SURA YA TANO

5.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

5.1 Utangulizi

Hii ni sura ambayo inafanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kama sehemu muhimu katika kukamilisha malengo ya utafiti wetu. Kwa kuwa huu ni utafiti linganishi tumefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa kuchukua kipengele fulani cha kifani ama maudhui na kukieleza namna kinavyotokeza katika kazi za washairi wawili walioteuliwa. Itakumbukwa kwamba, utafiti huu una jumla ya madhumuni mahususi matatu. Hivyo basi, katika uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti madhumuni hayo ndiyo yaliyozingatiwa na kwamba ndio yaliyoongoza uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data. Tunaanza kufanya uchambuzi wa data kwa kulichambua na kulijadili dhumuni mahususi la kwanza. Dhumuni hilo si lingine bali ni lile linalozungumza juu ya kutofautiana kwa vipengele vya kifani baiana ya washairi teule katika zao. Katika kufanya hivyo tumeanza na muundo katika ushairi wao kama ifuatavyo:

5.2 Muundo Katika Ushairi

Muundo ni mpangilio maalumu wa beti za shairi uliopangwa na msanii kwa nia ya kufikisha dhamira na maudhui mbalimbali kwa hadhira iliyokusudiwa kama ilivyokusudiwa (Njogu na Chimerah, 1999). Wanaendelea kueleza kwamba, katika wakati tulionao muundo wa ushairi ambao umekuwa na mashiko sana ni ule wa tarbia, yaani kila ubeti wa shairi kuwa na mistari minne yenye vina na mizani kumi na sita. Haji Gora Haji ni miongoni mwa washairi ambao wanaufuata na kuutumia

muundo huu wa tarbia katika utunzi wake wa mashairi. mfano mzuri ni huu tunaondoa hapa chini.

*Uchumi ukwamuliwe, ukwamuke kwa haraka
Ukwamuke hima uwe, ukae tunakotaka
Kabisa huko usiwe, kunako janga kutoka
Isiwe kuwekaweka, ukwamuliwe uchumi.*

Ubeti huu unajumla ya mistari minne ambayo yote kwa pamoja inawasilisha hoja kuhusu kuuinua uchumi na msomaji akisoma anaelewa kile kinachosemwa hasa ni nini. Ubeti huu haumuachi msomaji hewani badala yake unampa uelewa wa hoja iliyokamilika.

Aina hii ya muundo ndiyo inayotumiwa na washairi wengi wa kimapokeo na hivyo kuufanya kuwa ndiyo muundo rasmi wa ushairi wa Kiswhaili kwa mujibu wa wana mapokeo. Tukitazama mashairi ya Saadan Kandoro tunamwona akiutumia muundo wa aina hii katika mengi ya mashairi yake. Kwa mfano: Katika shairi la *Kujitawala Kugumu* anaeleza:

*Ni mume sio mwanamke, aliniambia fahamu,
Mtawaliwa mcheke, cheko ya kumlaumu,
na tena yapambazuke, kujitawala Kigumu
Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.*

Tunapotazama ubeti huu tunaona mshairi ametumia mistari minne katika kuujenga ubeti wake. Usomapo kazi za washairi wengine kama vile Mathias Mnyampala na wengineo utawaona nao wakiandika mashairi yao kwa kutumia aina hii ya muundo.

Wanausasa kwa upande wao wakiongozwa na Euphrase Kezilahabi wanasema kwamba shairi si lazima liwe na mistari mine katika kila ubeti ndiyo liwe shairi. Shairi linaweza kuwa na idadi yoyote ile ya mistari kutegemeana na nia na utaalumu

wa mshairi katika kutunga mashairi yake. Kwa mfano, katika shairi la *Mafuriko* anasema:

*Nitaandika wimbo juu ya mbawa za inzi
Utoe muziki arukapo wa usikie walio wengi
Ushairi wa jalalani utaimbwa
Juu ya vidonda vya wakulima
Na usaha ulio jasho lao
Nitaandika juu ya mbawa za wadudu
wote warukao.*

*Juu ya mistari ya pundamilia
na masikio makubwa ya tembo,
Juu ya kuta vyooni, maofisini, madarasani
Juu ya paa za nyumba na kuta za Ikulu!
Na juu ya khanga na tisheti
Nitaandika wimbo huu.*

Katika shairi hili Euphrase Kezilahabi ametumia mistari saba katika ubeti wa kwanza na mistari sita katika ubeti wa pili. Vile vile mistari ya beti hizi imeundwa kwa kipande kimoja tu na sio viwili kama ilivyo kwa Haji Gora Haji. Ingawa shairi hili limeandikwa kwa mistari mmoja linafikisha dhamira zilizokusudiwa kwa wasomaji wake pasipo shida yoyote. Katika msitari wa kwanza anasema “Nitaandika wimbo juu ya mbawa za inzi”, msitari wa pili “utoe muziki wa usikie walio wengi”. Mistari hii inatoa maana pale msomaji anaposoma lakini unapotaka kuimba shairi hili ama kulighani ni dhahiri kwamba itakuwa ni vigumu sana na hivyo kumkosesha ladha ya ushairi msomaji anayetaka kulisoma shairi hili kwa kuliimba. Massamba (1983) anasema kwamba shairi ni lazima liwe na muundo wake maalumu na ikiwa shairi linaandikwa kama barua tu hilo haliwezi kabisa kuitwa kuwa ni shairi. Anaendelea kueleza kwamba, ukitazama maana za ushairi zinazoelezwa na Kezilahabi (1974) na Topan (1974) utaona kwamba wanasema ushairi ni lazima uwe na muundo wa aina

fulani lakini hawauoneshi muundo huo katika mashairi. Kwa kufanya hivyo wanakuwa hawaandiki mashairi bali wanaandika Mapingiti kama asemavyo Mayoka (1984). Katika muundo kuna kipengele cha vina na mizani nacho kinatokeza kama sehemu muhimu ya muundo wa ushairi wa Kiswahili hasa ule wa kimapokeo.

5.2.1 Vina na Mizani Katika Ushairi

Massamba (1983: 102) anaeleza kwamba kina au vina kwa wingi ni ile silabi au pigo la mwisho wa msitari katika utenzi, au pigo la kati na mwisho wa msitari katika shairi la Kiswahili. Kazi kubwa ya vina katika mashairi ni kutoa msisitizo juu ya jambo ambalo mtunzi anataka jamii ama wasomaji wake walipate. Kwa kurudiarudia silabi ama sauti fulani katika ushairi basi inakuwa ni rahisi kwa msomaji kuinasa dhamira ama dhima fulani inayoelezwa na mtunzi.

Washairi wa kimapokeo akiwemo Haji Gora Haji amejitahaidi kutumia vina na mizani katika mashairi yake. Katika shairi la *Madanganyo* anasema:

*Tumefanya sote kazi, pori hilo kulifyeka
Na kuchimbua ardhi, shamba likakamilika
Mbona hamtuulizi, kuvuna kunapofika
Kuzichukuwa nafaka, mkazila peke yenu (Uk. 06).*

Ukiutazama ubeti huu wa shairi unaona kwamba mshairi anatumia vina kati “zi” na vina mwisho “ka” ambayo vinatoa msisitizo juu ya dhuluma inayofanywa na baadhi ya viongozi dhidi ya wananchi. Vina hivi vinaonesha hasira aliyonayo mdhulumiwa dhidi ya mdhulumu. Vile vile, vina hivi vinaonesha kwamba dhuluma ni kitu kibaya sana ambacho kinahatarisha upatikanaji wa haki za binadamu. Matumizi haya ya vina na mizani pia yanarahisisha zoezi la kuimbika kwa ushairi na msomaji anapata ladha ya ushairi huo.

Euphrase Kezilahabi kwa upande wake haandiki ushairi kwa kufuata urari wa vina na mizani. Anaandika hivi kwa sababu anaeleza kwamba, shairi si lazima liandikwe kwa kuzingatia urari wa vina na mizani ndiyo liitwe shairi. Mawazo haya yanaungwa mkono na Mulokozi (1975) pale anaposema kwamba, ushairi wa Kiswahili hautambuliki kwa vina na mizani bali utamaduni na lugha yake. Katika kuthibitisha mawazo haya Euphrase Kezilahabi ametunga mashairi ambayo hayafuati urari na vina na mizani. Kwa mfano: Katika shairi la *Mafuriko* anasema:

*Mti mkongwe umelalila upande
 Wa nyumba zetu hafifu
 Upepo mkali uvumapo hatulali
 Kila kukicha twatazama mizizi yake
 Na mkaao wake, na kuta hafifu za nyumba
 Lazima ukatwe kuanzia matawi hadi shina
 Mafuriko ya mwaka huu yaashiria
 Tutabaki kuwasimulia wajukuu
 Mwaka ule wa mafuriko
 Miti mingi mikongwe iliaanguka, (uk.4).*

Shairi hili halina urari wa vina wala mizani na wanusasa wanaliona hili kuwa ni shairi na si vinginevyo. Kandoro (1978) anaeleza kwamba, mashairi yanayoandikwa na Euphrase Kezilahabi ni mashairi lakini si mashairi ya Kiswahili. Ushairi wa Kiswahili unataratibu zake pamoja na miiko yake. Katika mashairi ya Euphrase Kezilahabi kunakosekana sifa muhimu ambazo ni vina na mizani. Mayoka (1984) anaeleza kwamba, vina na mizani ni uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Anaposema ni uti wa mgongo wa ushairi ana maana kwamba ni kitu muhimu sana ambacho kikikosekana basi ushairi huo hauwezi kuitwa ushairi wa Kiswahili.

Mawazo haya tunakubaliana nayo ingawa si kwa asilimia mia kwa mia. Tunasema hivi kwa sababu shairi linahitaji mambo mengi mpaka kukamilika kwake. Hivyo

kutoa hitimishi kwamba vina na mizani ndio uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili si sahihi sana. Kwa mfano, hata watunzi wa kimapokeo hawawezi kutunga mashairi yao kwa udhati unaopaswa kufuatwa katika kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo. Katika shairi la *Madanganyo* tunamuona Haji Gora Haji akiandika hivi:

*Tumefanya sote kazi, pori hilo kulifyeka
Na kuchimbua ardhi, shamba likakamilika,
Mbona hamtuulizi, kuvuna kunapofika
Kuzichukua nafaka, mkazila peke yenu (Madanganyo, uk.06).*

Katika msitari wa pili kuna kina “dhi” huku katika vina kati vingine ni “zi”. Hii inaonesha kwamba, mshairi huyu bado hajaiva katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili kwa kufuata kanuni za ushairi kama zilivyoainishwa na Abeid (1954). Abeid (1954) anaeleza kwamba ushairi wa Kiswahili unatungwa kwa vina ambavyo vinafanana katika ubeti mzima na siyo katika msitari unaofuata unatumia kina tofauti.

Kwa upande wa mizani, washairi wengi wakimapokeo wanatunga mashairi yao kwa kutumia mizani 16 katika msitari mmoja wa ushairi. Ukirejelea ubeti tuliondondoa hapo juu unaweza kuona kila msitari una jumla ya mizani 16 ambayo inamwezesha msomaji kuliimba shairi kwa uzuri kwa sababu lina uwiano wa mizani. Ukiyasoma mashairi ya Euphras Kezilahabi utabaini kwamba, mashairi hayo hayana mizani zinazowiana kama ilivyo kwa ushairi wa kimapokeo. Ukiwauliza wana usasa kuhusu hili watakujeleza kwamba, shairi si lazima liimbike bali shairi linatakiwa kutoa ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Mawazo haya yanapingwa vikali na Sengo pale anaposema:

Washairi wanaojiita kuwa ni wa kisasa, wanaandika ushairi. kwa sababu kuna baadhi ya sifa za ushairi zinajitokeza katika ushairi wao lakini wameingilia dhana. Waswahili wameeleza aina yao ya

ushairi kulingana na mazingira na utamaduni wao. Kutokana na hilo wakaweza kueleza maana ya ushairi kwamba unajumuisha hiki na kile. Sasa iweje mtu ambaye si Mswahili kuja na kuanza kutoa dhana ya ushairi wa Kiswahili? Kwa kufanya hivyo, ni sawa na kusema kwamba unapokuta mtu/jamii fulani wanayaita mazao fulani kwa jina la mahindi halafu wewe ukasema si mahindi ni maharagwe bila shaka utakuwa umekwisha haribu mambo”.

Haya ndiyo mawazo ya Sengo alipokuwa akitoa muhadhara kuhusiana na ushairi wa Kiswahili katika kongamano la Kiswahili lililoandaliwa na chuo Kikuu Huria cha Tanzania mwaka 2010.

5.2.2 Matumizi ya Kibwagizo

Kibwagizo ni yale maneno ambayo mtunzi wa ushairi anayotumia kama kituo katika ushairi wake. Washairi wa kimapokeo akiwemo Haji Gora Haji anatumia kibwagizo ambacho kinajirudiarudia katika ushairi mzima. Kwa mfano, katika shairi la *Wenye Vyao Watubana* anasema:

*Wenye vyao watubana, twaumia masikini
La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani
Kwa sasa kilo ya dona, bei mia ishirini
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana*

Katika ubeti wa pili nao anadika hivi:
*Washindana matajiri, kwa bei siyo utani,
Ni pigo kwa mafakiri, tulio hali ya chini
Wezeni kutafakari, wanyonge tu madhilani
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana, (uk.10).*

Katika beti hizi mbili na nyingine zinazoendelea tunaona kibwagizo kikurudiwarudiwa ktika kila mwisho mwa ubeti. Marudio haya nia yake hasa ni kumfanya msomaji akumbuke dhamira inayoelezwa katika shairi hilo. Hapa mshairi anamtaka msomaji afahamu kwamba, chochote asomacho katika shairi husika basi

akumbuke kwamba nia kuu ya shairi hilo ni ile inayoelezwa katika kibwagizo. Kwa mfano, katika beti mbili zilizopo hapo juu twaoneshwa kwamba; watu wa kipato cha chini wanaishi maisha ya chini kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali kutokana na mfumuko wa bei. Hivyo katika kibwagizo mshairi anatoa wito kwa viongozi kuhakikisha kwamba tatizo hili linashughulikia ili wananchi waweze kuishi maisha ya kuridhisha.

Kwa hivyo, kutoakana na matumizi ya kibwagizo hulifanya shairi kuwa rahisi kueleweka kwa msomaji hata kama yeye binafsi si mtaalamu wa kuhakiki mashairi kwa kutumia nadharia za uhakiki wa kifasihi. Inawezekana msomaji akashindwa kupata dhana ya shairi husika katika mistari mitatu ya mwanzoni mwa beti lakini akifika katika msitari wa mwisho ambao ni kibwagizo hutambua kwamba shairi lote linazungumza juu ya kitu gani. Kwa upande mwingine tunaweza kueleza kwamba, matumizi ya kibwagizo katika mashairi ni njia ya makusudi kabisa ya kusukuma mbele dhamira za shairi husika ili siwafikie wasomaji ama hadhira iliyokusudiwa.

Euphrase Kezilahabi haandiki beti za ushairi wake kwa kuziwekea kibwagizo kinachofanana. Kibwagizo kinakuwa ni tofauti katika kila ubeti. Isitoshe; kila kibwagizo ni kipande kimoja tu cha msitari si vipande viwili kwa msitari kama ilivyo kuwa Haji Gora haji. Euphrase Kezilahabi katika shairi la *Dhifa* anaandika:

*Ni chakula cha mchana,
Walanchi wameshafika,
Wazungu, Wahindi, Waarabu
Washateka sehemu zao
Chakula ki mezani
Nidhifa*

*Mawaziri wenye kula
Wabunge wapewa magari*

*Waandishi waliosajiliwa
 Watangazaji wenye yale yale
 Wakereketwa wasokereka
 Kimya wamekaa, (uk. 27).*

Hizi ni beti mbili za shairi moja lakini zinatofautiana katika kibwagizo chake. Kila ubeti una kibwagizo chake ambacho ni msitari mmoja tu ama nusu msitari. Kibwagizo cha aina hii hakimsadii msomaji kupata dhana ya shairi kwa haraka kwa sababu kila ubeti una kibwagizo chake, hali ambayo inamfanya msomaji wakati mwingine kuchanganyikiwa kutokana na kukutana na kitu kipya pale afikapo mwishoni mwa kila ubeti. Akifundisha katika mihadhara ya wanafunzi wa shahada za uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mulokozi (2011) anasema:

Wasomaji walio wengi ambao ni wa kiwango cha kawadia katika masuala ya uhakiki wa kifasihi hawaelewi ushairi wa Kezilahabi kwa urahisi kwa kuwa hauna kibwagizo kinachojirudiarudia katika kila ubeti kama ilivyo katika ushairi wa kimapokeo. Msomaji anakutana na jambo jipya katika kila ubeti na mpaka aweze kuunganisha mambo yote hapa na kuwa kitu kimoja basi inakuwa ni kazi ngumu sana.

Maelezo haya tunakubaliana nayo kwa asilimia mia kwa mia. Kwa wanafunzi wa shule za sekondari na wale wa ngazi ya shahada za awali huwa wanatoka patupu kabisa wasomapo mashairi ya mshairi huyu. Angalau kwa wanafunzi wa umahiri wanaweza kupata uelewa wa haraka katika mashairi ya Euphrase Kezilahabi baada ya kuwa na ujuzi kidogo kuhusiana na nadharia pamoja na mikabala ya uhakiki kwa kifasihi.

Kuna mahali fulani hapo nyuma tumeeleza kwamba Kezilahabi anaandika mengi ya mashairi yake kwa kutumia kipande kimoja tu cha msitari. Hata hivyo kuna mashairi

machache anaandika kwa kutumia, mistari mwili katika kuunda mshororo, mmoja wa ubeti. Kwa mfano: katika shairi litwalo *Karibu Ndani* lililopo katika diwani ya *Karibu Ndani* (1988) anasema:

*Na hiki kibanda gani, ghafla mbele yangu
Ni kibanda cha Msonge, mlango wake mmoja
Mlango wenye uwazi, na ndani moto wawaka,
Hodi hodi wenyewe, ni mimi kichwamaji
Natafuta zangu njuga, na lile vazi la Kindu
Ingawa sina ubuyu, naja kukesha nanyi (uk.34).*

Katika shairi hili Euphrase Kezilahabi anatumia vipande viwili katika kila mshororo na ubeti huu unajumla ya mishororo sita. Kibwagizo nacho katika ubeti huu wa shairi kimeundwa kwa vipande viwili vya mshororo. Baada ya kutoa maelezo marefu kuhusu muundo katika ushairi ni vema sasa tugeukie kipengele cha mandhari.

5.3 Mandhari Katika Ushairi

Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kwamba, mandhari ni mahali ambapo kazi ya fasihi inapotendelea ambapo inaweza kuwa mjini, kijijini, nyumbani, shuleni, kanisani au msikitini na kadhalika. Kwa mantiki hii tunaweza kueleza kwamba, mandhari inaweza kuwa ya namna mbili yaani mandhari halisi na isiyo halisi. Haji Gora Haji ni miongoni mwa watunzi wanaotumia mandhari halisi katika mashairi yake huku Euphrase Kezilahabi akitumia zaidi mandhari dhahania. Mashairi mengi ya Haji Gora Haji yanakuwa na mandhari halisi kwa mfano: Katika shairi la *Ukokolewe* (uk.5) anaeleza kuhusu mandhari ya Tanzania kwa namna mbalimbali. Anaandika kuwa:

*Utalii tuukuze, uzidi kuimarika
Uimarike uweze, nafasi hiyo kushika*

*Ushike na uingize, madata kuminika
Iwe kwa kila dakika, wauinue uchumi*

*Ukulima ni msingi, kwa dhati tukiushika
Utapolima kwa wingi, nafaka bila kuchoka
Na matunda kila rangi, yatakayonunulika
Kwa madala si shilingi, na kuchangia uchumi*

*Uvuvi ule wa leo, ambao uliofika
Kuendelezwa na huo, pia inahitajika
Unao wake upeo, kwa uchumi kunyanyuka
Na juhudi zatakika, kwa kuokoa uchumi.*

Katika beti hizi tatu tunaona mshairi akifafanua aina mbalimbali za mandhari zinazopatikana hapa Tanzania. Kwanza anaonesha kwamba kuna mandhari nzuri kwa ajili ya kuvutia utalii na hiyo kuliwezesha taifa kujipatia fedha za kigeni. Vivutio hivyo ni pamoja na mbuga za wanyama, mlima Kilimanjaro, na sura ya nchi pamoja na uoto wake kwa ujumla.

Katika ubeti unaofuata anaonesha kwamba, hapa nchini kuna ardhi nzuri kwa ajili ya kilimo cha mazao kama vile nafaka na matunda ya aina mbalimbali. Katika nchi hii kuna upatikanaji wa matunda katika maeneo mengi ikiwemo Tanga katika maeneo ya Lushoto na Muheza, Morogoro, Mbeya, Mkuranga na kadhalika. Vile vile, anaonesha kwamba hapa nchini kuna mandhari nzuri kwa ajili ya kilimo cha nafaka za aina mbalimbali. Maeneo yanakubali kilimo cha nafaka hapa nchini ni mengi kupita yale yanayokubali kilimo cha matunda. Iwapo wananchi watafanya juhudi katika kilimo cha mazao stahiki kwa kila eneo ni dhahiri kwamba, matatizo ya njaa yatakuwa ni historia. Ni jambo la ajabu kukuta jamii ya Kitanzania inalia njaa hali ya kuwa kuna ardhi ya kutosha kuzalisha chakula kwa ajili ya wananchi wote.

Katika ubeti wa mwisho anaonesha kwamba, nchini Tanzania kuna mandhari nzuri kwa ajili ya uvuvi. Mandhari hii inasadifiwa kutokana na kuwepo kwa mito, maziwa na bahari za kutosha kuwapatia wananchi kitoweo na pia kuuza sehemu ya kilichovuliwa ili kujipatia kipato cha kutosha kuendeshea maisha yao ya kila siku.

Aina zote hizi za mandhari inayosawiriwa na Haji Gora Hoji ni mandhari halisi inayopatikana katika nchi ya Tanzania. Kwa mujibu wa Haji Gora Haji mandhari hii ni muafaka katika kuunyanyua uchumi wa nchi ya Tanzania na watu wake. Jambo hili halina shaka kwa kuwa ni la kweli na dhati kabisa. Hata hivyo, Haji Gora Haji amesahau kwamba, kuwa na mandhari nzuri kama hii peke yake haitoshi kuwa sababu ya kuuokoa uchumi. Yapo mambo mengine ambayo yanapaswa kutekelezwa kwanza ili mwishoni mwa siku mandhari hii nzuri iweze kuwanufaisha wananchi na kuinua uchumi wa nchi. Miongoni mwa mambo yanayopaswa kuimarishwa ni upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wananchi katika gharama ambazo wanaweza kuzimudu. Pili wapatiwe elimu ya kutosha kuhusiana na namna shughuli zote za uchumi tulizozitaja hapa zinapaswa kutekelezwa ili wazifanye shughuli hizo kwa tija na ufanisi. Kwa kiasi kikubwa mambo haya hayafanyiki kwa kiwango kinachopaswa na hivyo kumfanya Mtanzania kuwa masikini wa kutupa pamoja na kuwa tajiri wa rasilimali mbalimbali tulizozitaja hapo awali.

Euphrase Kezilahabi kama tulivyoeleza hapo awali kwamba, yeye anatumia zaidi mandhari ya kinadharia kuliko mandhari halisi. Mandhari hii inajitokeza pia katika kazi mbalimbali za riwaya alizotunga. Kwa mfano, katika shairi la *Matumaini* anasema:

*Akiyumbayumba
Na sarawili zee mawinguni*

Kama mlevi mwenye mguu mmoja, nilimwona
Akitoka magharibu kwenda mashariki
Kisha akaanguka baharini kwa kishindo
Binadamu tukasubiri. Tukasubiri
Halafu baharini ndege katoka
Karuka juu mawinguni
Wengine wakasema: Ndiye!
Wengine: Siye!
Tukasubiri (uk. 06).

Katika ubeti huu kunajitokeza matumizi ya mandhari dhahania. Mandari kama vile ya mawinguni, mlevi mwenye, mguu mmoja na kadhalika ni sehemu tu ya mandhari dhahania inayotumiwa na Euphrase Kezilahabi katika shairi hili. Ingawa mandhari hii ni dhahania inasawiri maisha halisi ya wananchi hasa katika kipindi cha Azimio la Arusha wananchi waliahidiwa kupata maisha mazuri iwapo watalikubali na kuliunga mkono Azimio la Arusha. Hata hivyo, maisha yao hayakubadilika kwa kiwango walichotegemea/walichoahidiwa na wengi wao wakijikuta wanaishi maisha duni kuliko ilivyokuwa kabla ya kuanzishwa kwa Azimio hilo la Arusha.

Hata hivyo, maelezo haya ya Euphrase Kezilahabi kuhusu Azimio la Arusha yanayojitokeza katika shairi la matumaini hayana mashiko ya kuweza kukubaliwa kitaaluma kwa kuwa ni ya jumla mno. Si kweli kwamba wananchi walipata maisha ya taabu sana katika kipindi cha Azimio la Arusha. Ukweli ni kwamba ni katika kipindi cha Azimio la Arusha ndimo wananchi wote kwa pamoja bila ubaguzi wa dini, rangi na kadhalika waliweza kupata elimu kwa usawa. Vile vile, huduma za afya zilipatikana kwa urahisi kwa wananchi wote tena karibu na maeneo yao ya kuishi. Hivyo kutoa maelezo kwamba, wananchi waliishi maisha ya taabu katika kipindi cha Azimio la Arusha si sahihi sana. Jambo ambalo tunaweza kukubaliana

nalo ni kwamba katika kipindi cha hali ngumu ya uchumi duniani ndipo wananchi waliishi maisha ya taabu kutokana na kuadimika kwa bidhaa mbalimbali yakiwemo mafuta ya kuendeshea magari na mitambo katika soko la dunia. Kuadimika kwa bidhaa hii kulisababisha kuadimika kwa bidhaa nyingine kama vile chakula, mavazi, vifaa vya ujenzi na kadhalika ambavyo vinategemea uwepo wa usafirishaji ili usafiri kutoka sehemu za uzalishaji kwenda sokoni, ama kwa walaji. Hili ndilo lililotokea na kuchangia katika kukwamisha harakati za Azimio la Arusha katika kuwaletea wananchi maisha bora. Hata hivyo suala la kwamba Azimio la Arusha limeleta maendeleo ama la ni suala la kimjadala na hivyo tunaliacha wazi kwa ajili ya mjadala mpana zaidi.

5.4 Matumizi ya Misimbo Katika Ushairi

Misimbo ni ishara zinazotumiwa na watunzi mbalimbali wa kazi za fasihi katika ujengaji wa dhamira na maudhui ambayo wanataka yawafikie wasomaji wao (Wamitila, 2002). Wamitila (2002) anaendelea kueleza kwamba, kuna misimbo ya aina tano ambayo ni msimbo wa kihemenitiki, msimbo wa kimatukio, msimbo wa kiutamaduni, msimbo wa kiseme na msimbo wa kirejelezi.

Washairi wawili tunaoshughulikia kazi zao wanatumia aina hizi za msimbo katika mashairi yao, ingawa kuna aina fulani ya msimbo inachomoza zaidi kwa mtunzi mmoja na kwa mingine inachomoza aina nyingine ya msimbo. Mshairi Haji Gora Haji kwa mfano anatumia msimbo wa kimatukio katika kujenga dhamira za ushairi wake. Katika shairi la *Vielezeo* anasema:

*Ukimwi vielelezo, vyake vinaendeleza
Mtu hasa ni wa mwanzo, yule anajituliza*

*Hupata maambukizo wengine kuwanukiza
Hiyo njia, moja wapo, inasambaza Ukimwi (uk. 3).*

Katika ubeti huu mshairi anaeleza matukio mbalimbali ambayo yanasababisha maambukizo ya Virusi vya Ukimwi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine. tukio la kwanza analolieleza ni lile la mtu kutotulizana na kuamua kufanya umalaya ama ukahaba na hivyo kujikuta ameshanasa katika maambukizi ya ugonjwa huo hatari. Tukio jingine ni hili:

*Damu nayo huchangia, pasi na kuichunguza
Yenye vidudu vibaya, mwingine kumwuongeza
Kuona wasaidiya kumbe wamuangamiza
Na hilo ni mojawapo, lisambazalo Ukimwi (uk.3).*

Hapa linaelezwa tukio jingine ambalo linachangia katika maambukizi ya Virusi vya Ukimwi. Nalo si jingine bali ni kumuongeza damu ambayo tayari ina virusi vya ugonjwa huo mgonjwa anayehitaji kuongezwa damu mwilini. hapa mshairi anaonesha matukio ya kizembe yaliyokuwa yanafanywa na wauguzi na madaktari kwa kumuongeza mgonjwa damu bila kuifanyia vipimo ili kuona kama ni safi isiyo na vijidudu vya Ukimwi au la. Ukisoma mashairi mengi ya Haji Gora Haji utaona anatomia aina hii ya msimbo katika ushairi wake zaidi kuliko aina nyingine ya msimbo ingawa misimbo mingine inaweza kutokeza hapa na pale katika baadhi ya mashairi yake.

Naye Euphrase Kezilahabi anatomia misimbo ya aina mbalimbali katika mashairi yake ili kujenga dhamira ambazo anataka ziifikie hadhira aliyoikusudia. Hata hivyo, msimbo wa kirejelezi ndio hasa unaotawala katika sehemu kubwa ya ushairi wake. Msimbo huu unatumiwa na msanii kueleza jambo fulani huku yeye mwenyewe

akiwa anamaanisha jambo jingine tofauti na maandishi yanavyoeleza. Kwa mfano, katika shairi la *Jibwa* anasema:

Jibwa likitoka jikoni
Ulimi lajilamba
Piga limekwiba piga
Jibwa likishika hatamu
Haliwezi kuacha utamu, (uk.15).

Katika ubeti huu “Jibwa” ni neno lililotumiwa kiurejeleza kuwahusu baadhi ya viongozi na wanasiasa ambao hawajali wananchi wao bali matumbo yao na yale ya familia zao. Jibwa ni mbwa aliyepita mipaka ya udokozi na kufikia hatua ya kuwa si mwizi tu bali jambazi wa kuogopewa na watu. Kama hivyo ndivyo ni dhahiri kwamba, wanasiasa wamefikia hatua ya kufanya ufisadi mkubwa wa kuwaibia wananchi rasilimali zao na kuwacha wakiendelea kutaabika na umasikini. Katika miaka ya hivi karibuni hapa Tanzania kumeibuliwa ufisadi wa hali ya juu katika Akaunti ya Madeni ya Nchi za Nje (EPA) pamoja na mkataba hewa wa RICHMOND, Kampuni ya uzalishaji Umeme wa dharura ambayo ilikuwa inachota mabilioni ya fehda kila siku pasipo kuzalisha umeme kwa tija na ufanisi hapa nchini.

Tukitazama aina mbili hizi za msimbo tulizokwisha kuzieleza tunabaini kwamba: Msimbo wa kimatukio uliotumiwa na Haji Gora Haji haumpi msomaji kazi kubwa ya kutafakari ili kufumbua maana ya shairi lililowasilishwa mbele yake ili aweze kuainisha dhamira zinazotokeza katika shairi husika. Katika shairi la *Vielezo* msomaji anaelewa mara moja ni dhamira gani ambayo mtunzi ameilenga imfikiye yeye msomaji. Kwa upande wa Euphrase Kezilahabi tunaona kwamba, aina ya msimbo ambayo ameitumia inamtaka msomaji kutumia muda mrefu kuitafakari

dhamira iliyokusudiwa na msomaji. Shairi la *Jibwa* haliko wazi Kama lile la Vielezo katika kueleza dhamira kwa msomaji wake. Msomaji wa ushairi wa Euphrase Kezilahabi ni sharti awe na ujuzi kidogo wa nadhari za uhakiki wa kifasihi ndiyo aweze kupata dhamira fulani katika shairi husika.

Ni vema ikafahamika kwamba Euphrase Kezilahabi ni mwanafunzi aliyekaa darasani akafunzwa nadharia mbalimbali za uhakiki wa utunzi wa kifasihi katika ngazi mbalimbali za taaluma ya fasihi ikilinganishwa na Haji Gora Haji. Hivyo nidhahiri kwamba, atatunga mashairi yake akiwa ameongozwa na nadharia hizo. Hii hata hivyo haiufanyi ushairi wake kuwa bora kuliko ushairi wa Haji Gora Haji bali ni suala la kimjadala ambalo linaachwa wazi kwa ajili ya kujadiliwa zaidi. Kutokana na hali hii Euphrase Kezilahabi anaonekana kutunga ushairi wake kwa ajili ya kundi fulani la wasomaji hadhira na si kila mtu anaweza kuusoma ushairi wake.

Kwa kufanya hivyo anaufanya ushairi wake kujitenga na sehemu kubwa ya wananchi kwa kuwa hawafahamu sana kuhusiana na mbinu na nadharia za uhakiki wa kifasihi anazotumia Euphrase Kezilahabi katika kutunga mashairi yake. Dhana ya kwamba ushairi ni mali ya jamii na unasawiri maisha halisi ya jamii inapotea na inakuwa haina makishiko ya kutosha kwa kuwa aina hiyo ya ushairi (wa Euphrase Kezilahabi) inawahusu watu wachache tu katika jamii. Sengo katika mazungumzo anaeleza kwamba:

Ushairi ama kazi nyingine yoyote ya kifasihi ni lazima isawiri maisha ya jamii kwa udhati wake na kila msomaji anayesoma aweza kuibua dhamira ama maudhui kulingana na jinsi alivyoelewa hata kama ni tofauti na aliyokusudia mtunzi. Sasa kama ushairi huo ama kazi yoyote ile ya fasihi inamtenga msomaji na kumfanya atoke

patupu kabisa asomapo shairi fulani eti kwa sababu si mjuzi wa nadharia za uhakiki wa kifasihi basi hiyo si fasihi ya Kiswahili bali ni fasihi nyingine kabisa.

Maleezo haya ya Sengo tunayaunga mkono kwa kuwa yanaeleza kwa udhati kuhusu maana na dhima ya ushairi na fasihi kwa ujumla katika jamii.

5.5 Matumizi ya Mafumbo Katika Ushairi

Senkoro (2011) anaeleza kwamba lugha ya mafumbo ni ile ambayo mtunzi wa kazi ya fasihi anaeleza mambo kwa kufichaficha pasipo kueleza kwa uwazi juu ya jambo husika. Anaendelea kueleza kwamba, aina hii ya lugha inajitokeza zaidi katika fasihi simulizi hasa katika utanzu wa hadithi. Hata hivyo si jambo la ajabu kukutana na aina hii ya matumizi ya lugha katika ushairi tena ushairi andishi. Washairi wote wawili wanatumia lugha ya mafumbo katika uwasilishaji wa dhamira mbalimbali. Hata hivyo, tumebaini kwamba Haji Gora Haji anatumia aina ya mafumbo anavyo tunaweza tukaiita mafumbo jumui na Euphrase Kezilahabi anatumia aina ya mafumbo ambayo tunaweza kuiita mafumbo nafisia yaani yanamlenga mtu binafsi.

Tukianza na Haji Gora Haji katika shairi la *Kimbunga* anaeleza:

*Kimbunga mji wa Siyu, kilichowahi kufika
Si kwa yule wala huyu, ilikuwa patashika
Kimeing'oa mibuyu, minazi kunusurika
Nyoyo zilifadhaika*

*Nyumba kubwa za ghorofa, siku hiyo zimeruka
Zikenenda kwa masafa, kufikia kwa kufika
Vibanda vyao malofa, vyote vikasalimika
Nyoyo zikafadhaika, (uk.01)*

Katika beti hizi kunaielezwa mambo mengi lakini kubwa hapa ni fumbo linaonesha kiwango cha utabaka kilichopo katika jamii hii. Wapo watu matajiri ambao

wanafananishwa na mibuyu na wapo masikini ambao wanalinganishwa na minazi. Fumbo jingine linaloelezwa hapa ni lile linalohusu utokeaji wa machafuko na athari zake. Fumbo hili linasema kwamba, pale wananchi wanapochoka kutendewa uonevu na viongozi wao huamua kutokeza hadharani kupigania haki yao. Iwapo hilo litokea masikini huwa hawajali kitu kwa sababu hawana cha kupoteza ikilinganishwa na matajiri ambao wana mali za aina mbalimbali. Sasa mshairi anawataka viongozi na wasiasa ambao ndiyo matajiri kuhakikisha kwamba, wanafanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa kiwango cha utabaka kilichopo nchini kinapungua ama kinaondoka ili kuepusha kimbunga yaani machafuko yasije yakatokea.

Euphrase Kezilahabi kwa upande wake anatumia mafumbo nafsi kwa sehemu kubwa ya ushairi wake. Katika shairi la *Matumaini* anaeleza hivi:

*Akiyumbayumba
Na sarawili zee mawinguni
Kama mlevi mwenye nguvu mmoja
Akitoka magharibi kwenda mashariki
Kisha akaanguka bahari kwa kishindo
Binadamu, tukasubiri. Tukasubiri
Halafu baharini ndege katoka
Karuka juu mawinguni
Wengine wasema: Ndiye!
Wengine Siye!
Tukasubiri*

Katika ubeti huu wa shairi anasemwa kiongozi mkuu wa nchi ambaye alifanya uamuzi wa kubadili sera za nchi pasipo kuwashirikisha wananchi wote. Kwa kufanya hivyo sera alizozidumisha zilishindwa kumkomboa mwananchi na badala yake zikamzidishia umasikini kwa kiwango kingine kikubwa zaidi. Matumizi ya mafumbo aina hii yaliwahi kumsukuma Frolova (2003) kueleza kwamba, Euphrase Kezilahabi

hazungumzii siasa katika *Karibu Ndani* (1998) bali anaeleza juu ya masuala ya watu binafsi. Frolova (2003) alishindwa kuelewa kwamba ni fumbo tu limepigwa kumrejelea mtu binafsi lakini masuala ya kisiasa bado yapo palepale.

Kwa ufupi haya ndiyo mambo ambayo katika utafiti huu tumeyaona kwamba yanawatofautisha washairi hawa wawili hasa katika vipengele vya fani ya ushairi kwa ufupi lakini kwa kukidhi mahitaji ya utafiti wetu. Vipo vingine ambavyo vinaweza kuelezwa katika kuonesha tofauti zinzojitokeza katika utunzi wa washairi hawa wawili lakini kwa muktadha wa utafiti huu intaosha kufikia hapa tulipofikia. Sasa tutazame vipengele vinavyowafananisha washairi wateule.

5.6 Matumizi ya Lugha ya Taswira

Taswira ni picha wanavyoipata wasomaji wa kazi ya fasihi pale wanaposoma kazi fulani ambayo inaweza kuwa ushairi, riwaya ama tamthilia. Euphrase Kezilahabi anatumia lugha ya taswira katika mashairi yake yaliyo mengi kwa mfano, katika shairi la *Karibu Ndani* anasema:

*Na hiki kibanda gani, ghafla mbele yangu
Ni kibanda cha msonge, mlango wake mmoja
Ni mlango wenye uwazi, na ndani moto wawaka
Hodi Hodi wenyewe, ni mimi kichwa maji
Natafuta zangu njuga, na lile vazi la kindu
Ingawa sina ubuyu, naja kukesha nanyi, (uk.34).*

Katika ubeti huu tunapata taswira mbalimbali zinazoeleza juu ya masuala ya utamaduni wa mwafrika kwa kutumiwa kwa maneno kama vila njuga, ubuyu na msonge katika ubeti huu wa shairi. Hii ina mkumbusha msomaji kwamba kama yeye yupo mjini basi afahamu kwamba wenzake aliowaacha kijijini bado wanaendeleza

utamaduni na yeye huko huko mjini pia aendelee kuutekeleza na kuuendeleza utamaduni wa Mtanzania usije ukapotea.

Taswira nyingine inayotokeza katika ubeti huu ni ile inayoeleza umasikini ambao bado unaendelea kuwasakama wananchi walio wengi hapo Tanzania. Ni dhahiri kwamba katika kipindi kama hiki bado kuna Watanzania wanaendelea kuishi maisha ya taabu katika nyumba za msonge. Nyumba hizi ni hatari kwa afaya zao ambazo ziko mahali ambapo wanaweza kupata maambukizi ya malaria, kung'atwa na wadudu hatari kama vile nyoka na nge miongoni mwao. Hii yote inatokana na sera mbaya za serikali katika kuhakikisha kwamba kila mwananchi anakuwa na maisha mazuri. Tunasema sera mbaya kwa sababu tunaona zinatungwa sera za nyumba ambazo zinawanufaisha viongozi wa ngazi za juu serikalini peke yao. Kwa mfano, hapa majuzi kumekuwa na vuguvugu la kuuza nyumba za serikali. Nyumba hizo wamegawiana viongozi wenyewe na baadhi ya watu wenye uwezo kifedha huku wananchi masikini wakiambulia patupu. Hii ndiyo taswira inayotokeza katika shairi la *Karibu Ndani* (uk.34).

Naye Haji Gora Haji anaonekana kutumia lugha ya picha na ishara katika mashairi yake pale anapoandika shairi la *Punda* (uk.21) anasema:

*Punda kakosa thamani, sababu vitimbi vyake
Milele akawa duni, wala asiheshimike
Kwa wake umuhimu, kavunjiwa hadhi yake
Ndiyo tabia ya punda, kurusharusha mateke
Kuchunga akikushinda, mwachie aende zake.*

Punda hakumbuki wema, hata kwa mchungu wake
Humpa mwinga mtama, na maji anufaike

Katu haiwi salama, shukurani zake mateke
 Ndiyo tabia ya punda, kurusha rusha mateke
 Kuchunga akikushinda, muwachiye ende zake

Katika beti hizi mbili tunapewa taswira ya mtu ama mtoto ambaye hathamini taabu wanazopata na walizowahi kuzipata wazazi wake katika kipindi chote cha kumlea. Kutothamini huko kunaonekana pale ambapo anaonya na kukatazwa kufanya mambo ambayo si mazuri lakini hasikii na kuamua kufanya kinyume na maelekezo ya wazazi wake. Watoto ama watu wa aina hii wapo wengi katika jamii na mwisho wao daima huwa ni mbaya.

Taswira nyingine inayotokeza katika beti hizi za shairi ni ile inayoonesha kuwa wanadamu baadhi yao hawana shukurani. Unaweza ukawasaidia sana lakini mwisho wa siku wakafanya jambo ambalo huwezi kuamini kama kweli anaweza kufanya hivyo. Wapo watu ambao wamesaidiwa na ndugu, jamaa ama marafiki kwa namna mbalibmali mpaka wakafika hapo walipofika. Lakini shukurani yao ni mateke kama yale ya punda. Imetokea mtu anamtukana na kumkashifu yule ambaye alimsaidia mpaka kufika hapo alipofika. Aina hii ya maisha si nzuri na inafaa kukomeshwa ili kuwapa haki wale ambao bado wanahitaji kusaidiwa ili wapate haki yao. Tunasema haki yao kwa sababu mtu anayesaidia watu wenye shida anaweza kukatishwa tamaa na hawa wasio na shukurani na kuona kwamba kila mtu hana shukurani na hivyo kuona kwamba hakuna haja ya kuendelea kuwasaidia watu wenye shida.

5.7 Matumizi ya Wahusika Kifasihi Simulizi

Wahusika wa kifasihi simulizi ni wale ambao si viumbe wenyewe uwezo wa kutenda matendo ya kibinadamu lakini wanapewa sifa hizo (Wamitila, 2008). Wahusika wa

aina hii wamekuwa wakitumiwa sana katika fasihi simulizi hasa katika ngano. Hata hivyo wahusika wa aina hii wanatokeza katika mashairi ya washairi hawa wawili. Euphrase Kezilahabi katika shairi lake la *Mafuriko* anatumia wahusika wa kifasihi simulizi pale anaposema:

*Nitaandika wimbo juu ya mbawa za inzi,
 Utoe muziki ambapo wausikie walio wengi
 Ushairi wa jalalani utaimbwa
 Juu ya vidonda vya wakulima
 Na usaha ulio jasho lao
 Nitaandika juu ya mbawa za wadudu
 Wote warukao
 Juu ya misitani ya pundamilia
 Na masikio makubwa ya tembo
 Juu ya kuta vyooni, maofisini, madarasani
 Juu ya paa za nyumba na kuta za ikulu
 Na juu ya khanga na tisheti
 Nitaandika wimbo huu.*

Katika ubeti huu Euphrase Kezilahabi anataja wahusika wa aina mbalimbali wa kifasihi simulizi. Wahusika hao ni inzi, pundamilia, tembo na wadudu wote warukao kama vile vipepeo, nyuki na kadhalika. Euphrase Kezilahabi anatumia wahusika hawa kufikisha ujumbe kwa hadhira kwamba rushwa imeenea na kutapakaa katika sehemu kubwa ya nchi na hivyo wananchi wanapaswa walifahamu hilo na kisha watizame njia muafaka za kutatua tatizo hilo. Pundamilia ni mnyama mwenye mistari myeupe inayong'aa na kumtambulisha popote pale alipo. Hivyo wimbo wa rushwa utakapoandikwa katika mistari hiyo ni dhahiri kwamba kila mtu ataiona na ataichukia. Masikio ya tembo ni makubwa sana kiasi kwamba kila mtu anaweza kuliona sikio la tembo hata kama akiwa mbali kiasi gani. Hivyo kuandika masuala yahusuyo rushwa katika masikio ya tembo ni wazi kwamba yatawafikia watu wengi.

Sehemu nyingine katika shairi la *Jibwa* tunamuona Euphrase Kezilahabi akimtumia muhusika “mbwa” kuwasawiri viongozi wasio waadhilifu. Anasema:

Jibwa likitoka jikoni
Ulimi lajilamba
Piga limekariba piga
Jibwa likishika hatamu
Haliwezi kuacha utamu, (uk. 05).

Jibwa ni chuku iliyotumiwa kuonesha mbwa aliyekubuhu katika wizi na udokozi wa chakula popote pale anapokiona. Mhusika huyu anatumiwa kurejela viongozi mafisadi na wala rushwa kwamba kutokana na wizi huo kuzoeleka imekuwa ni sehemu ya maisha yao na kamwe hawawezi kuacha tabia hiyo mbaya. Kutokana na hali hiyo Euphrase Kezilahabi anawataka wananchi kuwa makini na viongozi wa aina hii kwa kutowapatia kura pale wanapokuja katika chaguzi mbalimbali ili kuwapatia fundisho.

Naye Haji Gora Haji ameandika mashairi yake na kutumia aina hii ya mhusika wa kifasihi simulizi. Wahusika kama vile punda, paka, kasa, chuwi na kadhalika wametumiwa kuwasilisha dhamira mbalimbali. Katika shairi la *Paka* (uk.22) anasema:

Paka nakuasa wizi, wacha kuiba samaki,
Imekuwa yako kazi, majikoni huondoki
Haufai uchokozi, si kizuri kitu hiki
Paka nakuasa wizi, vitoweo usiibe

Shairi hili halitofautiani snaa na lile la *Jibwa* (uk.05) katika maudhui yake. Hata hivyo shairi hili linaeleza juu ya udokozi, wizi na ufisadi uliokithiri kama ilivyo kwa Euphrase Kezilahabi ambaye amezungumzia ufisadi katika shairi la *Jibwa*. Shairi la

Paka linawaonya watoto wenye tabia ya kufanya udokozi wa vitu nyumbani kuacha tabia hiyo mara moja ili kuwa watu wema katika utu nzima wao. Wala rushwa na mafisadi anao wawezeza Euphrase Kezilahabi katika shairi la *Jibwa* walianza kidogo kidogo kama paka kwa kudokoa vitu vidogo vidogo na baadaye wakaingia katika kutenda ufisadi mkubwa. Kwa hali hii Haji Gora Haji anawataka wazazi kuhakikisha kwamba, watoto wao wanafunzwa maadili yatakayowaepusha na kitendo cha udokozi ili baadaye wasiwe wala rushwa wakubwa yaani mafisadi.

Wahusika hawa wa kifasihi simulizi wametumiwa na washairi hawa wawili kutenda matendo ya kibinadamu na kumuwezesha mchambuzi kudadavua maana mbalimbali za kifasihi zinazo wasilishwa na wahusika hao na kuonesha kwamba ni kweli wamesawiriwa wakitenda matendo ya kibinadamu.

5.8 Matumizi ya Ucheshi Katika Ushairi

Hii ni mbinu ya kisanaa ambayo msanii anaitumia kwa kueleza matukio ambayo yana chekesha pale msomaji asomapo shairi au kazi yoyote ile ya fasihi. Wakati mwingine msanii anatumia maneno ya utani na mzaha ili kumfanya msomaji acheke pale anaposoma kazi fualni ya fasihi. Kwa mfano katika ubeti huu wa Euphrase Kezilahabi anasema:

Azimio sasa ni mabaki ya chakula
Kwenye sharubu za bepari
Kalamu inayovuja
Katika mfuko wa mwanafunzi
Vumbi zito
Baada ya ng'ombe kupita
Kilichosalia sasa
Ni punje za ulezi

Zilizosambazwa jangwani

Na mpandaji kipofu, (Shairi hili ni Azimio, uk. 27).

Tunaposoma shairi hili kwa makini tunaona lugha ya ucheshi ikijitokeza na inatufanya tucheke pale tunaposoma. Senkoro (2011) anaeleza kwamba, matumizi ya lugha ya ucheshi hayamfanyi msomaji aचेके tu halafu inaishia hapo bali inamfanya atafakari baada ya kucheka ili kuelewa ni dhamira gani zinazowasilishwa na mshairi katika shairi husika. Kwa mfano, pale anaposema “Azimio ni mabaki ya chakula kwenye sharubu za bepari”, anatumia watu tunaolifahamu Azimio la Arusha tucheke kwanza. Baada ya kucheka tunajiuliza swali, inakuwaje mshairi anafikia hatua ya kulifananisha Azimio la Arusha na mabaki ya chakula katika sharubu za bepari. Hii inaonesha kuwa Azimio limekuwa haliwezi tena kutekeleza yale lililokusudia kutokana na kushindwa na nguvu ya ubepari na mabepari.

Mashairi Haji Gora Haji naye anatumia mbinu ya ucheshi katika kuwasilisha dhamira na maudhui mbalimbali kwa jamii iliyokusudiwa. Katika shairi la *Kibwangai* tunakutana na aina ya ucheshi pale ambapo mmoja wa nyani alikatwa mkia wake ili aonekane kama binadamu pale ambapo ataingia maskanini mwa binadamu naye kufanya shughuli ya kilimo. Hata hivyo, baada ya nyani huyo kufanikiwa kutimiza adhima hiyo aliwageuka wenzake kwa kutowapatia sehemu ya mazao aliyovuna na kujinufaisha yeye binafsi. Wenzake walikasirishwa na hali hiyo na ndipo walipoamua kumrudishia mkia wake. Anasema:

Mkia baada kumpa, mambo yakawa mabaya

Nguo zake kazitupa, unyani kumrudiya

Kaanza kuchupa chupa, mitini akarukiya

Akafanana na wenzake, akiwa nyani katimu

*Wenzake wakamcheka, wote na kumzomeya
Akakosa la kushika, kwa haya kujioneya
Majuto yakamfika, akabakia kuliya
Akarudia porini, iliko yake kaumu*

Hadithi hii inamfanya msomaji acheke kwanza pale anapokutana nayo kwa mara ya kwanza. Baada ya kucheka ndipo anaanza kujiuliza maswali kama vile, hii hadithi inafunza juu ya jambo gani? Baadaye anatambua kwamba, hadithi hii inazungumza juu ya kutimiza ahadi uliyokwisha itoa mbele ya wale uliowaahidi. Viongozi mbalimbali katika kipindi cha uchaguzi hasa madiwani na wabunge wamekuwa wakiahidi kutenda mambo mbalimbali ambayo hata hivyo hawawezi kuyatekeleza tena kwa makusudi tu. Hata hivyo, katika sehemu nyinyi wananchi bado hawajaelimika vya kutosha kiasi cha kuwaadabisha viongozi wa aina hii kama walivyofanya nyani kwa nyani mwezao. Wananchi wengi hasa wa maeneo ya vijijini bado wanaendelea kuwachagua viongozi wale wale ambao wanawadanganya kuwa watawaletea maendeleo, kumbe wanajiletea maendeleo wao wenyewe na familia zao. Baadhi ya maeneo ya mjini wananchi wameanza kuamka kwa kasi na kuacha kuwachagua viongozi ambao hawatekelezi ahadi za kuwaletea wananchi maendeleo na kuwapigia kura wale ambao wanaamini kwamba wataleta maendeleo katika jamii.

Hali hii imeshuhudia vugu vugu la mabadiliko ya kisiasa pale ambapo baadhi ya viongozi wa chama tawala waliposhindwa na kuangushwa katika chaguzi mbalimbali zikiwemo zile za wabunge. Jambo hili linatukumbusha msemu usemao “Ahadi ni deni” na kama ilivyokopeshwa ndivyo itakavyolipwa”. Hapa viongozi wa sasa wanakumbushwa kutekeleza wajibu wao pamoja na ahadi wanazozitoa kwa wananchi ili yasiwakumbe yale yanayotokea kwa baadhi ya wenzao. Nao pia

wakitekeleza ahadi zao itakuwa si tu mtaji wao wa kisiasa bali itakuwa ni namna bora ya kuwaharakishia wananchi maendeleo.

5.9 Mwingiliano Matini

Mbinu ya mwingiliano matini inatumiwa sana na watunzi wa kazi mbalimbali za fasihi pale ambapo tanzu zaidi ya moja zinapojitokeza katika beti za mashairi yao, ama kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili. Haji Gora Haji ameichukua hadithi ya *Kibwagai* na kuiwasilisha katika mfumo wa shairi. Shairi hilo linaanza hivi:

*Kuna hadithi ya kale, kwa babu nimepokeya
Kwa manyani zama zile, mkasa ulotokeya
Nilikuwa mwanakale, hiyo miaka zingatiya
Leo nawadokezeya, kwa nilivyoyafahamu.*

*Nyani baada kugunduwa, watu wanawaviziya
Sababu yake kwa kuwa, hila yao mimea
Na ndipo wakaamua, mwenzao kumtumiya
Ende akawalimiye, mazao yalo muhimu.*

Moja kwa moja mtu asomapo shairi hili anagundua kwamba, ni hadithi inasimuliwa lakini kupitia njia ya ya ushairi. Huu ndiyo mwingiliano wa tanzu yaani ushairi na hadithi vimewekwa pamoja, hadithi imeingia katika ushairi. Haji Gora Haji alitaka kufikisha ujumbe tuliosema wa kuhakikisha kwamba, wananchi wanakuwa na tabia ya kutekeleza ahadi zao pindi wanapo ahidi kufanya hivyo. Iwapo hawatatekeleza ahada hizo kwa wakati si tu kwamba wananchi hawatawachagua tena bali pia itakuwa wanawacheleweshea wananchi maendeleo yao.

Mshairi Kezilahabi anayetumia mwingiliano wa tanzu katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa kama ilivyokusudiwa katika shairi lake la *Azimio* (uk. 27)

tunaona anaeleza Azimio la Arusha ambalo hili ni tukio la kihistoria katika kazi ya fasihi kwa namna ya masimulizi ya kihadithi. Kwa mfano anaeleza:

*Azimio sasa ni mabaki ya chakula
Kwenye sharubu za bepari
Kalamu inayovuja
Katika mfuko wa mwanafunzi
Vumbi zito
Baada ya ng'ombe kupata
Kilichosalia sasa
Ni punje za ulezi
Zilizosambazwa jangwani
Na mpandaji kipofu, (uk. 27).*

Tunapolisoma shairi hili tunaliona kwamba ni la kihistoria na tena ni masimulizi ya kihadithi. Kwa hivyo hapa kuna mwingiliano wa utanzu wa hadithi, taaluma ya historia na ushairi. Viwili vya mwanzo vimeingia katika ushairi ili kuwalisiliha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira iliyokusudiwa.

5.10 Udokezi Kuhusu Dhamira

Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kwamba dhamira ni yale mawazo makuu ambayo yanawasilishwa na mtunzi wa kazi ya fasihi kwa hadhira iliyokusudiwa ili aidha waburudike ama wapate mafunzo fulani yatakayo waongoza katika maisha yao. Washairi wote wawili tuliowateua wamezungumza juu ya dhamira mbalimbali katika mashairi yao. Miongoni mwa dhamira hizo ni ile ya uongozi katika jamii. Euphrase Kezilahabi ametunga mashairi kama vile *Mke wa Waziri* akionesha kwamba, viongozi wanapopata mamlaka na madaraka wanawasahau wananchi wao wakifanya kila linalowezekana katika kujenga na kuimarisha maisha yao. Anasema hivi:

Sikiliza Monika
Sisi tumezoea vituko vya wakubwa
Huyu mumeo anatoka kijiji jirani
Tulimwona akilambwa na mbwa
Alipomaliza kujisaidia
Na alikimbia siku ya tohara
Sasa naye avuta kidevu shingo upande
Kama beberu, tayari kupigana
Wewe Monika
Twende ufukweni kuogelea
Tuone hiyo cheni ya dhahabu.

Tunaposoma ubeti huu tunabaini kwamba viongozi wengi wanapopata mamlaka ya uongozi hupata utajiri wa haraka haraka hali ya kuwa wao walikuwa ni masikini wa kutupa kabla ya kupata mamlaka hayo. Anamchora mke wa waziri kuwa sasa anayo cheni ya dhahabu ambayo ndiyo anaivaa kiunoni badala ya ushanga aliokuwa anaivaa hapo zamani kabla ya mume wake kupata uongozi.

Vilevile, katika ubeti huu mshairi anaonesha kwamba, hata mume ambaye ndiye waziri mwenyewe hakuwa na uwezo mkubwa wa mali na fedha kabla ya kupata nafasi ya uongozi aliyonayo hivi sasa. Baada ya kuupata uongozi ametajirika na kuwa tajiri mkubwa ambaye tena bila aibu anawadharau watu maskini na kuwaona si lolote si chochote. Hii ndiyo tabia ya viongozi wengi wa kisiasa mara tu baada ya kupata uongozi. Euphrase Kezilahabi anaendelea kueleza katika shairi hilo kuwa:

Wewe Monika
Ulitoka kwetu bila ushanga kiunoni
Kama kumbikumbi asi mbawa
Ulipojika mjini ukaolewa na waziri
Sasa wataka tusimame barabarani
Kukupungia matawi mabichi
Upitapo wainua kipua juu

*Chogo limechongoka kama senene
Aendaye kwenye harusi ya mende
Na kutusanifu kwa mawani meusi
Kama nyani achezaye sarakasi
Unajua kuchekecha, (uk. 13).*

Hapa Euphrase Kezilahabi anaichora picha kamili ya mwanamke huyu namna alivyokuwa hapo awali na maisha yake yalivyo hivi sasa. Hii yote inaonesha ubinafsi waliona viongozi wetu katika kujilimbikizia mali huku wakiwaacha wananchi wanaishi maisha duni na taabu kubwa.

Haji Gora Haji ameliona hili na anawaasa viongozi kwamba waache tabia hiyo mara moja kwani saa yoyote wananchi watakapoamua ni rahisi kwa viongozi hao kuondolewa madarakani na pengine kuchukuliwa hatua kali. Katika shairi la *chaka* anaeleza hivi:

*Yao makubwa majambo, wakitendea wenzao
Huzimwaga zao kumbo, kwa zilivyo hila zao
Na kubadilishia umbo, iwe kama kwamba sio
Lakini ni ole wao, wanao macho waona*

Katika ubeti huu mshairi anaufananisha uongozi kuwa ni sawa na chaka. Chaka ni mahali ambapo mtu ama mnyama anaweza kujificha na mtu mwingine asiweze kumuona kwa urahisi. Hivyo viongozi wapo katik nafasi za uongozi walizopo kwa dhamana ya wananchi. Kama ni chaka kwa maana kwamba wanaweza kujichukulia mali na rasilimali nyingine za umma kwa urahisi tu na watu wengine ama wananchi wasiweze kuwaona. Kwa hili anawaeleza kwamba wananchi wa leo waona vizuri kupitia mbadiliko ya ghafla na ya kila siku yanayotokea katika maisha yao hususani katika maendeleo ya kifedha na mali nyinginezo.

Haji Gora Haji anawaona viongozi kama watu muhimu sana ambao hawapaswi kujiingiza katika masuala ya wizi na dhuluma kwa wananchi na badala yake kuwa wao ndio watetezi wa wananchi wa hali za chini za kimaisha. Hili analionesha katika shairi la *Wenye vyao watubanwa*. Anasema hivi:

*Wenye vyao watubana, twaumia masikini
La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani
Kwa sasa kilo ya dona, bei mia ishirini
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana*

Katika ubeti huu mshairi anaonesha kwamba, viongozi ndio ngao ya utetezi wa watu wa hali za chini pale ambapo kunatokea matatizo kama ya kupanda bei za bidhaa kwa ghafla. Viongozi watawatetea wananchi kwa namna mbalimbali ukiwemo ile ya kupunguza kodi katika bidhaa na vile vile kudhibiti mfumuko wa bei kupitia taasisi zake. Hii ndiyo kazi ya viongozi na ndiyo maana wananchi wanawachagua ili wafanye kazi hiyo.

Hata hivyo, Haji Gora Haji amesahau kwamba wenye biashara hizo ambazo zinapandisha bei ya bidhaa kila uchao ni za watu wale wale ambao ndio viongozi. Bidhaa kubwa kama vile zile zinazohusiana na masuala ya mafuta kwa mfano zinamilikiwa na viongozi nchini kwa kushirikiana na wafanyabiashara wakubwa. Hivyo kuwaeleza ama kuwaona kama viongozi hao ni watetezi wa watu masikini ni kujidanganya kwa sababu ni vigumu sana kwao kutekeleza udhibiti huo wa bei kwa sababu wananufaika nao. Akiendeleza dhamira yake ya kuwaonya viongozi kwamba waachane na maovu wanayowafanyia wananchi katika shairi la *Kimbunga* (uk.01) anasema:

*Kimbunga mji wa Siyu, Kilichowahi kufika
Si kwa yule wala huyu, ilikuwa patashika,*

*Kimeing'owa mibuyu, minazi kunusurika
Nyoyo zilifadhaika.*

*Nyumba kubwa za ghorofa, siku hiyo zimeruka
Zikenenda kwa masafa, kufikia kwa kufika
Vibanda vyao malofa, vyote vikasalimika
Nyoyo zilifadhaika.*

Hapa ana watahadharisha viongozi kwamba, wasiwatendee uovu wananchi kwani siku wananchi watakapokasirika hali itakuwa mbaya tena mbaya sana. Iwapo wananchi watakasirika na fujo ikatokea ni dhahiri kwamba, watakaopata hasara ni wale watu matajiri na walaji wa rasilimali za nchi si wale masikini. Anaposema *Kimbunga* kitavunja maghorofa, na majabali halafu kitabakisha nyumba za miti ana maana hiyo tuliyoisema kwamba atakayepata hasara ni mtu tajiri kwa sababu masikini hana cha kupoteza. Kimbunga kikali kinapotokea hakiwezi kuacha kubomoa nyumba za ghorofa peke yake na kuacha nyumba dhaifu. Hii inaonesha kwamba, nyumba za miti hata zikiangushwa gharama yake ni kidogo tu na baada ya muda mfupi zinaweza kujengwa tena kwa kutumia gharama kidogo sana ikilinganishwa na nyumba za ghorofa.

Kutokana na mfano huu mshairi anawataka viongozi kuamka, kufungua macho yao na kuanza kuchapa kazi kama inavyopasa ili wasiweze kuwapa wananchi hasira ambayo itawafanya wapate imani ya kisaikolojia kwamba hata kama tukiingia vitani ili kuwatoa madarakani viongozi wa sasa hatuna kitu cha kupoteza bali wao viongozi ndio ambao watapoteza mali na utajiri wao walioupata kwa kuwaibia wananchi, mali na rasilimali zao. Dhamira nyingine inayoelezwa na washairi teule ni ile inayohusu masuala ya rushwa.

5.11 Rushwa Katika Jamii

Rushwa ni hali ya kiongozi ama mtumishi wa umma ama wa sekta binafsi kudai kiasi fulani cha fedha au jambo jingine lolote ili aweze kumpatia huduma mtu yoyote anayehitaji huduma hiyo tofauti na utaratibu uliowekwa na unaotambulika. Nchini Tanzania kwa mfano, rushwa imekuwa ikipigwa vita tangu enzi za awamu ya kwanza ya serikali mpaka leo. Pamoja na kupigwa vita huko rushwa bado ipo na inaendelea kurudisha nyuma maendeleo ya taifa. Katika diwani ya *Dhifa* Euphrase Kezilahabi anaonesha namna viongozi wa ngazi za juu wanavyokula rushwa katika masuala ya uwekezaji kwa kuiuza nchi na rasilimali zake kwa wawekezaji wa kigeni.

Anasema:

*Ni chakula cha mchana,
Wananchi wameshafika
Wazungu Wahindi, Waarabu
Weshateka sehemu zao
Chakula ki mezani
Ni dhafa, (uk. 27).*

Katika ubeti huu wa shairi anawataja wawekezaji ambao ndiyo wanaonekana kuwa na uwezo wa kutimiza vigezo vya kufanya uwekezaji kuwa ni Wahindi, Wazungu na Waarabu na hakuna mahali anawataja Waafrika kama nao ni sehemu ya wawekezaji. Viongozi wa serikali wanawakubali wawekezaji wa aina hii kwa sababu wanatoa rushwa kubwa kwa viongozi wanaohusika na kutoa vibali vya kuruhusu uwekezaji huku mwekezaji mzawa akionekana kuwa hana fedha ya kutoa rushwa kubwa ikilinganishwa na wageni hao. Katika ubeti unaofuata anataja makundi ya viongozi ambao ndio wanahusika katika utoaji wa idhini ya wawekezaji wa kigeni kuwekeza hapa nchini. Anasema:

*Mawaziri wenye kula
Wabunge wapewa magari
Waandishi waliosajiliwa
Watangazaji wenye yaleyale
Wareketwa wasokereka
Kimya wamekaa, (uk.27).*

Katika ubeti huu anawataja wabunge, mawaziri na sifa zao. Mawaziri wanatajwa kuwa ni wapenda kula. Euphrase Kezilahabi hakutaja hicho chakula wanachopenda kula ni kipi? Bila shaka ni rushwa ambayo wanapewa na wawekezaji ili waweze kupitisha mikataba yao kwa kutia saini. Iliwahi kutokea hapa nchini waziri mmoja aliposaini mkataba wa kuiruhusu kampuni fulani kuchimba madini hapa nchini katika hoteli moja huko Ulaya bila hata ya kuusoma na kuuelewa kwanza mkataba huo unahitaji jambo gani, lipi la kuondolewa, kurekebishwa ama kubadilishwa ili mkataba huo uweze kulipatia taifa tija ya kusukuma mbele maendeleo ya taifa. Mkataba huo uliosainiwa hotelini ulionesha kwamba mwekezaji atanufaika zaidi kuliko serikali kutokana na uwekezaji huo. Haji Gora Haji naye ameisawiri dhamira ya rushwa katika shairi la rushwa pale anaposema:

*Rushwa kajenga kambi, na kuondoka hataki
Afanya kila vitimbi, mkaidi hashikiki
Tumzushieni wimbi, isiwe kutuhiliki
Tumchimbie handaki, rushwa tukamzikeneni,
(uk. 12).*

Katika ubeti huu wa shairi, mshairi anaonesha kwamba rushwa imeenea na kukua sana kiasi cha kuweza kuonekana kama ni kitu cha kawaida katika jamii. Rushwa kujenga kambi maana yake ni kwamba imekomaa ama imeshaota mizizi kiasi kwamba juhudi za kupambana nayo zinahitaji kuimarishwa ipasavyo. Miongoni mwa hatua za kuchukua katika kuitokomeza rushwa ni pamoja na kukataa kutoa ama

kupokea rushwa katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Anasema, rushwa inapaswa kuchimbiwa handiki na kufukiwa moja kwa moja isionekane katika uso wa ardhi. Haji Gora Haji anaamini kwamba rushwa inaweza kutokomezwa kama kila mwananchi ataamua kufanya hivyo. Kwa mfano, mtu akiombwa rushwa asipewe na anayetaka kutoa rushwa basi ikataliwe yaani isipokelewe na ikiwezekana taarifa zipelekwe katika vyombo husika ili aweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Hata hivyo, tunayaona mawazo haya kuwa ni mazuri na yana mchango muhimu katika kusiadia harakati za kupambana na rushwa. Kwa kiasi fulani hatukubaliani na mawazo haya kwa kuwa hayaja bainisha sababu za watu kudai na kutoa rushwa hazija bainishwa na namna ya kuziimarisha ama kuzipatia ufumbuzi sababu za rushwa. Ili kuweza kupambana na rushwa ni lazima sababu za kutoa ama kupokea rushwa ziiainishwe vizuri ili mwisho wa siku mambo yanende vizuri kama inavyopasa. Tume ya Jaji Warioba ya mwaka 1996 imeainisha sababu mbalimbali za kutoa na kupokea rushwa. Ukosefu wa elimu ya uraia miongoni mwa wananchi wengi kuna sababisha vitendo vya rushwa kuongezeka siku hata siku. Sababu nyingine ni ukosefu wa huduma za uhakika katika sekta za afya, umeme, maji na elimu na hivyo kumlazimu mwananchi atoe rushwa ili aweze kupata huduma nzuri tena kwa uharaka. Hizi ni baadhi tu ya sababu ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi na kisha kuwezesha harakati za kupambana na rushwa zina fanikiwa vizuri.

5.12 Hitimishi

Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji wanatofautiana kwa kiasi kikubwa katika kipengele cha muundo katika utunzi wa mashairi yao. Wakati Haji Gora Haji

anaandika mashairi ambayo yanafuata urari wa vina na mizani katika kila ubeti wa Shairi Lake Euphrase Kezilahabi hafuati kabisa utaratibu huo katika utunzi wa mashairi yake. Kwa hali hiyo mashairi ya Haji Gora Haji yanaimbika kwa urahisi na pia yanaeleweka kwa msomaji kwa uharaka ikilinganishwa na yale ya Euphrase Kezilahabi ambayo ni sharti kwa msomaji kuwa angalau na ujuzi kidogo katika nadharia za uhakiki wa kifasihi. Hata hivyo, mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji yanafanana katika matumizi ya lugha ya picha, mkato, ishara, taswira na matumizi ya wahusika wa kifasihi simulizi. Kwa upande wa dhamira tumeona kwamba washairi wote wawili wanazungumza juu ya utabaka, unyonyaji na rushwa katika jamii kama dhamira kuu katika kazi zao.

SURA YA SITA

6.0 HITIMISHI, MUHTASARI WA MAPENDEKEZO

6.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho katika tasinifu hii. Sura hii inahitimisha utafiti mzima na kutoa mapendekezo kwa ajili ya tafiti zijazo. Kwa msingi huo basi, tunaanza na kutoa muhtasari kisha hitimishi na mwisho ni mapendekezo.

6.2 Muhutajari

Utafiti huu umekamilika baada ya kupitia sura sita. Sura ya kwanza ilihusu utangulizi wa utafiti mzima ambao nia kuu ya kufanyika kwa utafiti huu ilitolewa. Katika sura hii tumeeleza kuhusu usuli wa mada ya utafiti ambao umeonesha kwamba, hakuna utafiti wa kina ambao umeshafanywa kuhusu kumlinganisha mshairi wa kimapokeo na yeyote yule wa kisasa. Usuli wa utafiti unaonesha kwamba kuna haja ya msingi ya kufanya utafiti wa kina ili kuona ni kwa vipi aina hizi mbili za ushairi zinatofautiana ama kufanana. Vile vile, katika sura hii pia tumeeleza tatizo la utafiti, Lengo kuu, madhumuni mahususi na maswali ya utafiti. Pia katika sura hii tumeeleza umuhimu wa utafiti mipaka ya utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti na mwisho ni mpango wa tasinifu.

Sura ya pili imefanya mapitiao ya kazi tangulizi zinazohusiana na anuani ya utafiti huu. Katika mapitiao haya tumeanza kwa kumtazama Euphrase Kezilahabi na watafiti watangulizi wanasema nini kuhusu mashairi yake. Wengi wa wanataaluma hawa wanamsifu Euphrase Kezilahabi kwamba, amefanya mapinduzi makubwa katika kuuletea ushairi wa Kiswahili muundo mpya wa utunzi. Muundo huo mpya ni

ule ambao haufuati urari wa vina na mizani. Miongoni mwao ni Topan (1974), Mulokozi (1975), Mulokozi na Kahigi (1979), Wamitila (2008) na Njogu na Chimeraha (1999). Kwa upande mwingine tumeweza kuwabaini baadhi ya watafiti na washairi wakimpinga Euphrase Kezilahabi katika utunzi wake wakitambua kwamba anatunga ushairi lakini si ushairi wa Kiswahili. Miongoni mwa wataalamu hawa ni Mayoko (1984), Kandoro (1978) na wengineo. Mawazo ya wataalamu wote hawa yamechukuliwa na kufanyiwa kazi katika tasnifu hii. Kwa mfano ni kutokana na kuwapo wale wanaopinga ushairi wa Kezilahabi na wengine wanaukubali ndiyo maana tukaona kuna haja ya kufanya utafiti wa kulinganisha na kulinganua mashairi ya kisasa na kimapokeo.

Sura ya tatu imewasilisha nadharia mbili ambazo ndizo zilizotoa dira na mwelekeo wa utafiti hu. Nadharia hizo ni Simiotiki na Umarx. Nadharia ya Simiotiki imetusaidia kuchambua misimbo mbalimbali ambayo ndiyo tuliyoitumia kulinganisha na kulinganua ushairi wa Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji. Nadharia ya Umarx nayo imetusaidia katika kuainisha masuala ya utabaka na unyonyaji unaofanywa na viongozi dhidi ya wananchi.

Sura ya nne imewasilisha mbinu na njia za utafiti mbinu hizo ni pamoja na usanifu wa utafiti, uteuzi wa kazi za kufanyia utafiti, populesheni na sampuli ya utafiti. Mbinu nyingine ni zile za ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mbinu hizi zimewezesha utafiti huu kukamilika kwa haraka na uhakika zaidi.

Sura ya tano imefanya uwasilishaji wa data na uchambuzi wake. Katika kukamilisha hili, tumechambua na kujadili data zinazoeleza juu ya kufanana baina ya Euphrase

Kezilahabi na Haji Gora Haji katika kueleza kwao masuala ya kifani. Mambo yaliyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na muundo wa ushairi, vina na mizani na masuala ya kibwagizo. Mambo mengine ni pamoja na matumizi ya lugha ya picha, ishara, taswira, ucheshi, lugha ya mafumbo na wahusika wa kifasihi simulizi. Mambo haya yameweza kufananisha na kutofuatisha utunzi wa washairi hawa wawili. Vile vile, tunaonesha baadhi ya dhamira zinazojitokeza katika mashairi haya kwa ufupi.

Sura ya sita ndiyo ya mwisho katika utafiti huu na inwezesha kufanya hitimishi, muhutasari na kutoa mapendekezo ya utafiti wetu kwa watafiti wanaokuja huko baadaye.

6.3 Hitimishi

Dhumuni mahususi la kwanza katika utafiti huu lililenga kulinganisha na kulinganua vipengele vya kifani katika ushairi wa Kezilahabi na Haji Gora Haji. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba Euphrase Kezilahabi anatunga mashairi ya Kisasa yasiyofuata mtiririko wa vina na mizani huku Haji Gora Haji akiandika mashairi yenye urari wa vina na mizani. Urari huo wa vina na mizani unamwezesha msomaji kupata msikiko wa dhamira ambao unamsaidia kuelewa kazi vizuri. Euphrase Kezilahabi anatunga ushairi usiofuata miundo ya kimapokeo kama vile tarbia ambao pia huufanya ushairi wake usiimbike kwa namna ile ya mashairi ya kisasa. Sengo (2012) katika mazungumzo amehitimisha kwa kueleza kwamba, mashairi ya kisasa yana sifa fulani za ushairi lakini si za ushairi wa Kiswahili. Kwa hali hiyo, ushairi wa kisasa usiofuata urari wa vina na mizani siyo ushairi wa Kiswahili.

Dhumuni mahususi la pili lililenga kuufananisha ushairi wa euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji katika vipengele vya fani. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji wanafanana katika vipengele vya wahusika wa kifasihi simulizi, ucheshi na matumizi ya tamathali za usemi. Kama wana usasa wanatunga mashairi yao kwa kutumia wahusika wa kifasihi simulizi ndiyo maana wanauita ushairi wao ni wa kisasa, mbona hata wanamapokeo nao wanatumia aina hiyo hiyo ya wahusika. Suala la usasa katika ushairi wa Kiswahili litaletwa na Waswahili wenyewe na siyo mtu wa kuja tu kutoka sehemu nyingine isiyo ya Waswahili.

Dhumuni mahususi la tatu lilihusu kudokeza dhamira zinazojitokeza katika mashairi ya washairi teule. Miongoni mwa dhamira zinazojitokeza katika mashairi ya wawili hawa ni pamoja na utabaka pamoja na rushwa na ufisadi.

6.4 Mapendekezo

Tunapendekeza utafiti ufanywe katika kuchunguza kama kuibuka kwa mashairi ya kisasa yalichangiwa na siasa ama maendeleo ya taaluma katika ngazi ya Chuo Kikuu ama la!

Tunapendekeza pia utafiti ufanyike kuhusu kuchunguza mabadiliko yanayotokea katika mashairi ya kimapokeo ili kuweza kuona kama yanasaidia kuupeleka mbele ushairi wa kimapokeo au hakuna maendeleo yoyote.

MAREJELEO

- Abeid, A., (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: EALB.
- Babbie, E., (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Bathes, R., (1994). *The Semiotic Challenge*. Berkely: University of California Press.
- Chandler, D., (1992). *Semiotics: The Basics*, London: Routledge Press.
- Chuwa, M., (2011). “Uchunguzi wa Vipengele vya Fani Katika Mashairi ya Mathias Mnyampala”. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Cohen, L. na Wenzke (2000). *Research Methods in Education* (5th end) London: Roulledge Press.
- Creswell, J.W., (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publication.
- Frolova, N., (2003). “Euphrase Kezilahabi: The Renewal of Kiswahili Poetry”. In *Kiswahili*, Vol. 66 Dar es salaam. IKR.
- Furlong, P. na Wenzake, (2000). *Research Methods and Statistics: An Integrated Approach*. New York: Harcourt College Publishers.
- Haji, G.H., (1994). *Kimbunga*. Dar es Salaam: TUKI.
- John, L., (2004). *Critical Reading: A Guide*. In [http://www. Brocku. Ca/English/jlge/criticalreadig. Html](http://www.Brocku.Ca/English/jlge/criticalreadig.Html). Accessed, 30th, October 2006.
- Juma, S.R., (2012). “Ufundishaji na Ujifunzaji wa Ushairi wa Kiswahili Katika Shule za Sekondari Jijini Dar es Salaam”. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kandoro, S., (1978), *Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili na Lugha Yake*. Dar es Salaam: Longman Ltd.

- Keys, B. na Wenzake (1989). "Four Faces of Fully Function Middle Manger;
California Management Review; Vol. XXIV. No, 4 pp. 59-67.
- Kezilahabi, E., (1974). *Kichomi*, Nairobi: Heinemann Educational books.
- Kezilahabi, E., (1977). "Mashari ya Saadan", *Mulika*, Namba 14. Dar es Salaam:
TUKI. Kur. 32-40.
- Kezilahabi, E., (1983). "Uchambuzi katika ushahi wa Kiswahili". Katika *Makala ya
Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*, Kur. 145-165. Dar es
Salaam: TUKI.
- Kezilahabi, E., (1988). *Karibu Ndani* Dar es Salam: DUP.
- Kezilahabi, E., (2008). Dhifa, Nairobi: Vide-Muwa.
- Kothari, C.R., (1992). *Reserch Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi:
Wiley Eastern Limited.
- Kothari, C.R., (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi:
New Age International Publishing Ltd.
- Massamba, D.P.B., (1983), "Suala la Ushairi wa Kiswahili". Katika Makala ya
Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili-Fasihi namba 3. Dar es
Salaam: TUKI.
- Mayoka, J., (1984). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Nairobi: EALB.
- Mlacha, A.K.S. na Madumulla, J.S., (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam:
DUP.
- Msokile, M., (1992). *Uhakiki: Karibu Ndani*. Dar es Salaam: DUP.
- Mulokozi, M.M., (1975). "Revolution and Reaction in Swahili Poetry". *In Kiswahili,
Vol. 45/2*. Dar es Salaam: IKR, Kur. 46-65.
- Mulokozi, M.M., (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha
Tanzania.

- Mulokozi, M.M. na K.K. Kahigi, (1979). *Kunga za Ushari na Diwani Yetu*, Dar es Salaam: TPH.
- Mulokozi, M.M. na T.S.Y. Sengo (1995). *History of Kiswahili Poetry [AD 1000-2000]*. Dar es Salaam: TUKI.
- Newman, W.L., (2006). *Social Reserch*. Sixth Edition, Boston: Pearson.
- Njogu, K. na Rocha, C., (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi, JKF.
- Nyangwine, N. na Masebo, J., (2002). *Uhakiki Katika Fasihi*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers
- Omary, M., (2011), “Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008), Tanisifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Robson, C., (2007). *How to do a Reserch Project: A guide for under graduate students*, Carton Victoria: Blackwell Publishing.
- Said, K., (2010). “Matumizi ya Lugha Katika Nyimbo za Harusi za Kabila la Wazigua. Utafiti mdogo wa Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Awali”, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Seleman, K. na Mtimbo, A., (2004), “Uhakiki wa Diwani ya Kimbunga”. Utafiti Mdogo wa Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Sengo, T.S.Y., (1994). “Utangulizi Katika *Kimbunga*”. Dar es Salaam: TUKI
- Senkoro, F.E.M.K., (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Topan, F., (1974). “Utangulizi katika *Kichomi*”, Nairobi: Heiremann.
- Wamitila, K.W., (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W., (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*,
Nairobi: Vide-Muwa.

Yin, R.K., (1994). *Case Study Research: Design ad Methods*, (2nd eds. Thousands
Oaks Calif: SAGE publishers.

Waliolejelewa Kupitia Mazungumzo

Mulokozi, M.M., (2009). *Mazungumzo Katika Mihadhara ya Umahiri Katika Fasihi*,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M., (2011), *Mazungumzo Katika Mihadhara ya Umahiri Katika Fasihi*,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sengo, T.S.Y., (2012), *Mazungumzo Katika Semina za Umahiri*, Chuo Kikuu Huria
cha Tanzania.

Senkoro, F.E.M.K., (2010), *Mazungumzo Katika Mihadhara ya Umahiri*, Chuo
Kikuu cha Dar es Salaam.

VIAMBATISHI

Kiambatishi Namba 1: Mashairi ya Haji Gora Haji yaliyotumika

Uchumi ukwamuliwe, ukwamuke kwa haraka

Ukwamuke hima uwe, ukae tunakotaka

Kabisa huko usiwe, kunako janga kutoka

Isiwe kuwekaweka, ukwamuliwe uchumi

Tumefanya sote kazi, pori hilo kulifyeka

Na kuchimbua ardhi, shamba likakamilika

Mbona hamtuulizi, kuvuna kunapofika

Kuzichukuwa nafaka, mkazila peke yenu (*Madanganyo*, uk. 06).

Tumefanya sote kazi, pori hilo kulifyeka

Na kuchimbua ardhi, shamba likakamilika,

Mbona hamtuulizi, kuvuna kunapofika

Kuzichukua nafaka, mkazila peke yenu (*Madanganyo*, uk.06).

Wenye vyao watubana, twaumia masikini

La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani

Kwa sasa kilo ya dona, bei mia ishirini

Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana (*Wenye vyao Watubana*, uk.10).

Washindana matajiri, kwa bei siyo utani,

Ni pigo kwa mafakiri, tulio hali ya chini

Wezeni kutafakari, wanyonge tu madhilani

Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana, (*Wenye vyao Watubana*, uk.10).

Utalii tuukuze, uzidi kuimarika

Uimarike uweze, nafasi hiyo kushika

Ushike na uingize, madata kuminika

Iwe kwa kila dakika, wauinue uchumi

Ukulima ni msingi, kwa dhati tukiushika

Utapolima kwa wingi, nafaka bila kuchoka

Na matunda kila rangi, yatakayonunulika

Kwa madala si shilingi, na kuchangia uchumi

Uvuvi ule wa leo, ambao uliofika

Kuendelezwa na huo, pia inahitajika

Unao wake upeo, kwa uchumi kunyanyuka

Na juhudi zatakika, kwa kuokoa uchumi (*Uokolewe*, 05).

Ukimwi vielelezo, vyake vinaendeleza

Mtu hasa ni wa mwanzo, yule anajituliza

Hupata maambukizo wengine kuwanukiza

Hiyo njia, moja wapo, inasambaza Ukimwi.

Damu nayo huchangia, pasi na kuichunguza

Yenye vidudu vibaya, mwingine kumwuongeza

Kuona wasaidiya kumbe wamuangamiza

Na hilo ni mojawapo, lisambazalo Ukimwi (*Vielezeo*, uk.3).

Kimbunga mji wa Siyu, kilichowahi kufika

Si kwa yule wala huyu, ilikuwa patashika

Kimeing'oa mibuyu, minazi kunusurika

Nyoyo zilifadhaika

Nyumba kubwa za ghorofa, siku hiyo zimeruka

Zikenenda kwa masafa, kufikia kwa kufika

Vibanda vyao malofa, vyote vikasalimika

Nyoyo zikafadhaika (*Kimbunga*, uk.01).

Punda kakosa thamani, sababu vitimbi vyake

Milele akawa duni, wala asiheshimike

Kwa wake umuhimu, kavunjiwa hadhi yake

Ndiyo tabia ya punda, kurusharusha mateke

Kuchunga akikushinda, mwachie aende zake.

Punda hakumbuki wema, hata kwa mchungu wake

Humpa mwingu mtama, na maji anufaike

Katu haiwi salama, shukurani zake mateke

Ndiyo tabia ya punda, kurusha rusha mateke

Kuchunga akikushinda, muwachiye ende zake (*Punda*, uk.21).

Paka nakuasa wizi, wacha kuiba samaki,
 Imekuwa yako kazi, majikoni huondoki
 Haufai uchokozi, si kizuri kitu hiki
 Paka nakuasa wizi, vitoweo usiibe (*Paka*, uk.22).

Mkia baada kumpa, mambo yakawa mabaya
 Nguo zake kazitupa, unyani kumrudiya
 Kanza kuchupa chupa, mitini akarukiya
 Akafanana na wenzake, akiwa nyani katimu

Wenzake wakamcheka, wote na kumzomeya
 Akakosa la kushika, kwa haya kujioneya
 Majuto yakamfika, akabakia kuliya
 Akarudia porini, iliko yake kaumu (*Kibwangai*).

Kuna hadithi ya kale, kwa babu nimepokeya
 Kwa manyani zama zile, mkasa ulotokeya
 Nilikuwa mwanakale, hiyo miaka zingatiya
 Leo nawadokezeya, kwa nilivyoyafahamu.

Nyani baada kugunduwa, watu wanawaviziya
 Sababu yake kwa kuwa, hila yao mimea
 Na ndipo wakaamua, mwenzao kumtumiya
 Ende akawalimiye, mazao yalo muhimu (*Kibwangai*).

Rushwa kajenga kambi, na kuondoka hataki

Afanya kila vitimbi, mkaidi hashikiki

Tumzushieni wimbi, isiwe kutuhiliki

Tumchimbie handaki, rushwa tukamziken *(Rushwa, uk.12)*.

Kiambatisho Namba 2: Mashairi ya Kezilahabi yaliyotumika

Nitaandika wimbo juu ya mbawa za inzi

Utoe muziki arukapo wa usikie walio wengi

Ushairi wa jalalani utaimbwa

Juu ya vidonda vya wakulima

Na usaha ulio jasho lao

Nitaandika juu ya mbawa za wadudu

wote warukao.

Juu ya mistari ya pundamilia

na masikio makubwa ya tembo,

Juu ya kuta vyooni, maofisini, madarasani

Juu ya paa za nyumba na kuta za Ikulu!

Na juu ya khanga na tisheti

Nitaandika wimbo huu.

Mti mkongwe umelalila upande

Wa nyumba zetu hafifu

Upepo mkali uvumapo hatulali

Kila kukicha twatazama mizizi yake

Na mkao wake, na kuta hafifu za nyumba

Lazima ukatwe kuanzia matawi hadi shina

Mafuriko ya mwaka huu yaashiria

Tutabaki kuwasimulia wajukuu

Mwaka ule wa mafuriko

Miti mingi mikongwe iliaanguka (*Mafuriko*, uk.4).

Ni chakula cha mchana,

Walanchi wameshafika,

Wazungu, Wahindi, Waarabu

Washateka sehemu zao

Chakula ki mezani

Nidhifa

Mawaziri wenye kula

Wabunge wapewa magari

Waandishi waliosajiliwa

Watangazaji wenye yale yale

Wakereketwa wasokereka

Kimya wamekaa (*Dhifa*, uk. 27).

Na hiki kibanda gani, ghafla mbele yangu

Ni kibanda cha Msonge, mlango wake mmoja

Mlango wenye uwazi, na ndani moto wawaka,

Hodi hodi wenyewe, ni mimi kichwamaji

Natafuta zangu njuga, na lile vazi la Kindu

Ingawa sina ubuyu, naja kukesha nanyi (*Karibu Ndani*, uk.34).

Akiyumbayumba

Na sarawili zee mawinguni

Kama mlevi mwenye mguu mmoja, nilimwona

Akitoka magharibu kwenda mashariki
 Kisha akaanguka baharini kwa kishindo
 Binadamu tukasubiri. Tukasubiri
 Halafu baharini ndege katoka
 Karuka juu mawinguni
 Wengine wakasema: Ndiye!
 Wengine: Siye!
 Tukasubiri (*Matumaini*, uk. 06).

Jibwa likitoka jikoni
 Ulimi lajilamba
 Piga limekwiba piga
 Jibwa likishika hatamu
 Haliwezi kuacha utamu, (*Jibwa*, uk.15).

Azimio sasa ni mabaki ya chakula
 Kwenye sharubu za bepari
 Kalamu inayovuja
 Katika mfuko wa mwanafunzi
 Vumbi zito
 Baada ya ng'ombe kupita
 Kilichosalia sasa
 Ni punje za ulezi
 Zilizosambazwa jangwani
 Na mpandaji kipofu (*Azimio*, uk. 27).

Sikiliza Monika

Sisi tumezoea vituko vya wakubwa

Huyu mumeo anatoka kijiji jirani

Tulimwona akilambwa na mbwa

Alipomaliza kujisaidia

Na alikimbia siku ya tohara

Sasa naye avuta kidevu shingo upande

Kama beberu, tayari kupigana

Wewe Monika

Twende ufukweni kuogelea

Tuone hiyo cheni ya dhahabu.

Wewe Monika

Ulitoka kwetu bila ushanga kiunoni

Kama kumbikumbi asi mbawa

Ulipofika mjini ukaolewa na waziri

Sasa wataka tusimame barabarani

Kukupungia matawi mabichi

Upitapo wainua kipua juu

Chogo limechongoka kama senene

Aendaye kwenye harusi ya mende

Na kutusanifu kwa mawani meusi

Kama nyani achezaye sarakasi

Unajua kuchekesha (*Mke wa Waziri*, uk. 13).